# UCHANGANUZI WA USEMI KATIKA NYIMBO ZA UKEKETAJI WA WANAWAKE KATIKA JAMII YA ABAGUSII WA KENYA

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

EGERTON UNIV
19 SEP 2013
P.O. BOX 536, EGERTON
ACQUISITION SECTION

MAGATO K. WILFRED

Tasnifu hii imewasilishwa kwa Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii katika kutimiza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili M.A (Kiswahili) katika Chuo Kikuu cha Egerton.

EGERTON UNIVERSITY

NOVEMBA 2010

EULIB
040 999

2013/96606

## UNGAMO NA IDHINI

### UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu. Haijawasilishwa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu chochote.

29-11-2010

**MAGATO K. WILFRED** — **TAREHE**

### IDHINI YA MTAHINI

Tasnifu hii ya uzamili imetolewa kwa idhini yangu kama msimamizi wa kazi hii aliyeteuliwa na Chuo Kikuu cha Egerton.

29.11.2010

**DKT. JAMES OGOLLA ONYANGO** — **TAREHE**

## HATILINZI

Hakuna ruhusa kunakili sehemu yoyote ya tasnifu hii kwa njia yoyote au kuhifadhi kwa namna yoyote bila ya idhini kutoka kwa mwandishi au Chuo Kikuu cha Egerton.

## TABARUKU

Naitabaruku tasnifu hii kwa wapendwa wafuatao: Baba mpendwa mzee John Okeyo, mke wangu mpendwa Jackline Monyangi pamoja na watoto wangu Kemunto, Moraa, Kebaso na Kerubo.

## SHUKRANI

Kwanza kabisa, ningependa shukrani zisizo kifani zimwendee msimamizi wangu Dkt. James Ogolla ambaye aliidurusu kazi hii bila kuchoka. Aliitwaa kama yake, akaisoma, akaniasa na kunielekeza kwa njia zote ili kuikamilisha kazi hii. Vilevile, shukrani nyingi ziwaendee wahadhiri wangu wote wa idara ya Fasihi, Lugha na Isimu ambao walinipokea kila nilipohitaji ushauri wao. Miongoni mwao ni Dkt Furaha Tchai, Dkt C. Kitetu, Dkt. Beja na mwalimu Gwachi Mayaka.

Isitoshe shukrani za dhati zimwendee mke wangu mpendwa Jackline Monyangi aliyenitia moyo wa kuendelea hata wakati matumaini yalipokuwa yanafifia. Pongezi pia ziwaendee ndugu yangu Simon Omosa na masahibu wangu wa dhati Mwalimu Nyamwaka na Mwalimu Makori ambao walinifaa kwa hali na mali.Wazazi wangu mzee John Okeyo na mama Rose Kerubo pia nawashukuru kwa malezi yao mema yaliyonifikisha ukubwani.

Orodha ya walioniauni ni ndefu; hivyo, wale ambao singeweza kuwataja japo walinisaidia, nawaambia, ahsanteni.

## ABSTRACT

This study sought to investigate the language used in female genital mutilation (FGM) discourse in the circumcision songs among the Abagusii community in Kenya. This is due to the fact that, despite the national and international campaigns against FGM, this practice lingers on in this community. Hence, this study sought to describe the language features used in FGM discourse, examine how social identities and relations are built through this discourse and the effects of the language used in nurturing this practice among the Abagusii. Ten circumcision songs were analyzed to shed light on the effect of language in regard to this practice. The study was based on Critical Discourse Analysis (CDA) theory, which looks at discourse in a three -dimensional approach, by looking at the relationship between text, discursive practice and the social practice. This theory embraces five tenets: That, discourse shapes and is shaped by society; discourse helps constitute (and change) knowledge, social relations and social identity; discourse is shaped by relations of power and invested in ideologies; the shaping of discourse is a stake in power struggles; and shows how society and discourse shape each other. These five tenets guided our research in congruence with our research objectives. Descriptive survey was used as our research design, whereby circumcision songs were recorded from focus group discussions for analysis as discourse texts. Tools for data collection included an interview schedule, a tape recorder and audio cassettes. A total of 16 circumcision songs were collected and 10 were purposively sampled as texts for analysis. Data analysis was done by describing the language features that included: repetition, metaphors, nouns, and adjectives. Three discursive strategies as proposed by Meyer and Wodak (2001:73) were adapted in the analysis of the social identities and relations amongst the circumcised and uncircumcised. They included: nomination, predication and argumentation. Our findings proved that indeed FGM has language features that promote it by creating social identities and relations that are positive for those who have undergone FGM and vice versa. It is hoped that the study will be of benefit to scholars interested in gender issues and oral literature; crusaders against FGM; and researchers in CDA.

# IKISIRI

Utafiti huu umeshughulikia matumizi ya lugha katika usemi wa ukeketaji katika nyimbo za ukeketaji katika jamii ya Abagusii nchini Kenya. Hii ni kwa sababu, ingawa kampeni kabambe za kitaifa na kimataifa zimefanywa kushutumu asasi ya ukeketaji kwa sababu ya madhara yake, bado ingali inashikiliwa na jamii hii. Utafiti huu ulidhamiria kufafanua sifa za lugha inayotumiwa katika usemi wa ukeketaji; kutathmini vile utambulisho wa jamii na mahusiano ya jamii yanavyojengwa kupitia usemi huu na kudhihirisha athari za lugha inayotumiwa katika kuendeleza ukeketaji miongoni mwa Abagusii. Kazi hii iliegemezwa katika nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi, ambayo huangalia mahusiano kati ya matini, maingiliano na muktadha kama pembe tatu za ujenzi wa usemi. Kwa kutumia nadharia hii utafiti huu umeegemezwa katika mihimili yake mitano:Usemi huundwa na jamii;Usemi husaidia katika kuunda (na kubadilisha) maarifa, mahusiano ya jamii na utambulisho wa jamii; Usemi huundwa na mahusiano ya kiuwezo na umesheheni imani(itikadi); Kuundwa kwa usemi ni swala kuu katika kinyang'anyiro cha uwezo/mamlaka; na jamii na usemi hujengana. Muundo wa utafiti wa uchunguzi wa kimaelezo ulitumika, ambapo nyimbo za tohara zilinaswa kutokana na mijadala ya vikundi teule ili kuchanganuliwa kama matini ya usemi. Nyimbo kumi na sita za ukeketaji zilikusanywa, ambapo kumi ziliteuliwa kimakusudi kama matini za kuchanganuliwa. Uchanganuzi wa data ulimulikia sifa za lugha zilizojitokeza: Takriri, jazanda, nomino na vivumishi. Mikakati mitatu ya uchanganuzi iliyopendekezwa na Meyer na Wodak (2001:73) ilitumika kuchanganua utambulisho wa kijamii na mahusiano ya kijamii kati ya waliotahiriwa na wasiotahiriwa. Mikakati hiyo ni: Unominoshaji, Uvumishaji na Kimjadala. Vyombo vya utafiti ni pamoja na kinasa sauti, kanda za kunasa sauti na mwongozo wa mahojiano. Matokeo ya utafiti wetu yalionyesha kuwa usemi wa ukeketaji una sifa za lugha zinazoukuza ukeketaji kwa kuwapa utambulisho wa kijamii ulio chanya wale waliokeketwa huku ukiwadunisha wanaoipuuza desturi hii. Kwa mfano waliokeketwa waliheshimiwa, wangeoleka, na husifiwa kuwa wao hukuza utamaduni. Ni matarajio yetu kuwa utafiti huu utawanufaisha wasomi katika maswala ya kijinsia na Fasihi Simulizi. Aidha, watafiti wanaoshughulikia uchanganuzi wa usemi watafaidika kwa kupata njia za kufanya uchanganuzi.

EGERTON UNIVERSITY LIBRA

## YALIYOMO

**UNGAMO NA IDHINI**....................ii
**HATILINZI**....................iii
**TABARUKU**....................iv
**SHUKRANI**....................v
**ABSTRACT**....................vi
**IKISIRI**....................vii
**YALIYOMO**....................viii
**ORODHA YA MAJEDWALI, GRAFU NA MICHORO**.................... x
**SHEREHE NA AKRONIMU**.................... xi
**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI**....................1
1.1 Usuli wa Mada....................1
1.2 Suala la Utafiti....................5
1.3 Madhumuni ya Utafiti....................6
1.4 Nadharia Tete....................6
1.5 Umuhimu wa Utafiti....................6
1.6 Upeo na Mipaka....................6
**SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDISHI**....................8
2.1 Utangulizi....................8
2.2 Ukeketaji wa Wanawake....................8
2.3 Msambao wa Kijiografia wa Ukeketaji....................9
2.4 Madhara ya Ukeketaji....................11
2.5 Sababu ya kuenzi Ukeketaji wa Wanawake....................13
2.6 Ufafanuzi wa Hatua za Ukeketaji wa Wanawake katika Jamii ya Abagusii....................14
2.7 Tafiti Zinazohusiana na Ukeketaji....................17
2.8 Lugha na Uwezo....................20
2.9 Msingi wa Nadharia....................21
**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI**....................26
3.1 Utangulizi....................26
3.2 Muundo wa Utafiti....................26
3.3 Mahali pa Utafiti....................26

3.4 Uteuzi wa Sampuli........................................................................................26
3.5 Uchanganuzi wa Deta........................................................................................27
**SURA YA NNE: UCHANGANUZI WA DETA........................................................29**
4.1 Utangulizi........................................................................................29
4.2 Sifa za Lugha katika Matini........................................................................................29
4.3 Ufasili wa Utambulisho wa Jamii katika Ukeketaji........................................................................................36
4.4 Matumizi ya Mikakati katika Ujenzi wa Utambulisho wa Kijamii........................................................................................37
4.5 Upambanuzi wa Athari za Lugha katika Ukeketaji........................................................................................52
4.6 Hitimisho........................................................................................58
**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO........................59**
5.1 Utangulizi........................................................................................59
5.2 Muhtasari na Hitimisho........................................................................................59
5.3 Matatizo Yaliyomkabili Mtafiti........................................................................................60
5.4 Mapendekezo........................................................................................60
**MAREJELEO........................................................................................62**
**VIAMBATISHO........................................................................................64**

## ORODHA YA MAJEDWALI, GRAFU NA MICHORO

### Majedwali

Jedwali 1: Msambao wa ukeketaji barani Afrika.........3
Jedwali 2: Msambao wa ukeketaji katika wilaya ya Kisii.........18
Jedwali 3: Mwingiliano kati ya matini na usemi.........37
Jedwali 4: Mikakati ya lugha katika ujenzi wa utambulisho.........38

### Grafu

Grafu 1: Nchi zilizo na asilimia 51-70.........10
Grafu 2: Nchi zilizo na asilimia zaidi ya 70.........10

### Michoro

Mchoro 1: Njia tatu za uchanganuzi wa usemi.........23

## SHEREHE NA AKRONIMU

| | |
|---|---|
| *Amabuko* | - Majani aliyoyalalia mtahiriwa. |
| *Ebirundu* | - Mimea inayochukuliwa kuwa takatifu ambayo aliyetahiri hupewa ashike ili damu isitoke nyingi. |
| *Egesa* | -Nyumba ndogo ambayo hukaa wazee. |
| *Egesagane* | - Msichana ambaye hajatahiri lakini anaendelea kuandaliwa kwa tohara. |
| *Ekemunu* | - Kikapu kidogo ambacho mtahiri hubebea vifaa vyake vya kazi. |
| *Ekemoya* | - Kikapu cha ngozi abebeacho vifaa mtahiri. |
| *Esaiga* | - Nyumba ndogo ambayo hukaa wazee au wavulana. |
| *Esuguta* | - Aina ya nyasi ambazo hupandwa kwa nyumba ya mtahiriwa ili aendelee kuinyunyizia maji akiwa ametengwa. |
| *Esimbore* | - Wimbo wa tohara. |
| *Enkuri* | - Anayelia anapotahiriwa huitwa jina hili. Hudharauliwa na kutengwa na wenzake. |
| Itikadi | - Jinsi mtu au kikundi cha watu kinavyouona ulimwengu. |
| *Obware* | - Sherehe ya kuvukisha msichana hadi utu uzima. |
| *Omware* | - Jina aitwalo msichana kuanzia siku ya tohara hadi anapofuzu. |
| *Omoiseke* | - Aliyefuzu sherehe zote za tohara. |
| *Enyaroka* | - Aliyefuzu sherehe zote za tohara. |
| *Omosegi* | - Mwalimu wa mtahiriwa hadi afuzu. |
| *Orotuba* | - Mahali pa kukeketea wasichana. |
| *Omosari* | - Anayetahiri wasichana. |
| *Omokebi* | - Anayetahiri wasichana. |
| Usemi | - Matumizi ya lugha iliyosemwa au iliyoandikwa kama tendo la jamii. |
| Ukeketaji | - Kuondoa sehemu fulani au sehemu zote za siri za wanawake. |

## AKRONIMU

| | |
|---|---|
| AIDS | - Acquired Immuno Deficiency Syndrome |
| CDA | - Critical Discourse Analysis |
| FGM | - Female Genital Mutilation |
| HIV | - Human Immuno Deficiency Virus |
| KDHS | - Kenya Demographic Health Survey |
| PATH | - Programme for Appropriate Technology in Health |
| UNICEF | - United Nations Children Fund |

# SURA YA KWANZA
# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Takribani wasichana milioni mbili wamo hatarini ya kukeketwa kote ulimwenguni. Karibu wasichana na wanawake 135 milioni ulimwenguni wamekeketwa. Wengi wao wanaishi Afrika, wachache Asia na wengine wanazidi kuongezeka Uropa, Kanada na Marekani ambao wanazidi kuteseka kutokana na athari ya ukeketaji wanawake. Wanawake hawa huhisi maumivu makali, kutokwa na damu, huambukizwa magonjwa na hata wengine hufa. Madhara haya huwasumbua kisaikolojia na hivyo huathiri hadhi ya wanawake na maisha yao ya kujamiiana.

Ukeketaji wa wanawake ambao kwa kawaida huitwa tohara ya wanawake, ni mfano wa jitihada za jamii ulimwenguni kukanya uwezo wa kike katika mambo ya kujamiiana, kuwadhibiti wanawake na kudhibiti njia zao za uzalio. Katika mataifa yaliyoendelea, kwa mfano , wanawake hufanyiwa upasuaji wa kiplastiki ili waongeze thamani yao ya kike.

Wanawake na wanaume barani Afrika na hata ulimwenguni wanaendelea kulalamikia hali ya ukeketaji katika juhudi za kuhakikisha umekomeshwa kabisa. Watu wajasiri na vikundi vya wasomi ndio watu wa kwanza wa kiAfrika ambao walivunja kuta za kiitikadi zilizozingira ukeketaji na kuanza kujadili swala hili. Makundi ya wasomi hasa yale ya madaktari yalisaidia kukusanya habari zaidi, hasa zinazohusu athari za kiafya, ambazo zinasaidia katika vita dhidi ya ukeketaji wa wanawake. Hivi leo, jamii nyingi za KiAfrika na KiAsia zinachuja tamaduni zao na kurekebisha itikadi huku wakishikilia mila zingine.

Juhudi za hivi karibuni katika kiwango cha kimataifa, hasa vyombo vya Umoja wa Kimataifa zimefanikiwa kuweka ukeketaji katika mada za afya na haki za binadamu asema Toubia (1993:6). Makundi haya huona ukeketaji kama janga la kiafya na njia ya kudhulumu wanawake. Kutoka kiwango cha kitaifa, serikali nyingi na viongozi wa kitaifa wamelaani hadharani ukeketaji, lakini ni wachache wamezua sheria zinazokana ukeketaji au hata mipango maalum ya kuwasihi watu kuacha ukeketaji.

Juhudi za kuukana ukeketaji, sharti zimulike katika utambulisho wa jamii wa wanawake na kubadilisha hali ya mwanamke kisaikolojia. Hii ni kwa sababu ukeketaji huzunguka wajibu wa mwanamke kijamii, kiimani, kiitikadi, mazoea ya kiafya, kuzaa watoto, kutosheka katika kujamiiana na maswala mengine ya mahusiano ya kijamii. Ubadilishaji wa mielekeo kuhusu ukeketaji utaleta mabadiliko katika hali ya kijumla ya mwanamke. Ukeketaji wa wanawake ni

jambo linalowahusu wanawake kwa wanaume ambao huamini usawa, heshima na haki kwa binadamu wote bila kujali uana, rangi, dini au kabila; usionekane kama tatizo la kikundi kimoja au utamaduni fulani, uwe wa KiAfrika , Kiislamu au Kikristo.

Katika bara la Afrika, mataifa 28 huendeleza ukeketaji. Nayo ni Benin ,Burkina Faso, Kameruni, Jamuhuri ya Afrika ya Kati, Chadi, Cote d' Ivoire, Djibouti, Misri, Uhabeshi, Eritrea, Gambia, Guinea, Guinea Bissau, Liberia, Mali, Mauritania, Niger, Nigeria, Senegal, Sierra Leone, Somalia, Sudan, Tanzania, Kenya na Ghana. Kulingana na Toubia (1993:25) takribani wanawake milioni 114 wamekeketwa barani Afrika, inavyodhihirishwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 1: Msambao wa Ukeketaji Barani Afrika**

| Nchi | Asilimia | Idadi halisi |
|---|---|---|
| Benin | 50% | 1,200,000 |
| Burkina Faso | 70% | 3,290,000 |
| Jamuhuri ya Afrika ya Kati | 50% | 750,000 |
| Chad | 60% | 1,530,000 |
| Cote d' Ivoire | 60% | 3,750,000 |
| Djibouti | 98% | 196,000 |
| Misri | 50% | 13,625, 000 |
| Uhabeshi na Eritrea | 90% | 23,940,000 |
| Gambia | 60% | 270,000 |
| Ghana | 30% | 2,325,000 |
| Guinea | 50% | 1,875, 000 |
| Guinea Bissau | 50% | 250,000 |
| **Kenya** | **50%** | **6,300,000** |
| Liberia | 60% | 810,000 |
| Mali | 75% | 3,112,500 |
| Mauritania | 25% | 262,500 |
| Niger | 20% | 800,000 |
| Nigeria | 50% | 30,625, 000 |
| Senegal | 20% | 750,000 |
| Sierra Leone | 90% | 1,935,000 |
| Somalia | 98% | 3,773,000 |
| Sudan (Kaskazini) | 89% | 9,220,000 |
| Tanzania | 10% | 1,345,000 |
| Togo | 50% | 950,000 |
| Uganda | 5% | 467,000 |
| Zaire | 5% | 945,000 |
| **JUMLA** | | **114, 296, 900** |

Asili: Toubia (1993:25)

Mokaya (2001:24) adai kuwa tafiti za maendeleo ya wanawake na *Programme for Appropriate Technology in Health* (PATH) nchini Kenya zinadhihirisha kuwa takribani makabila 30 kati ya 42 huendeleza ukeketaji. Miaka ya kutahiri hubadilika kutoka kabila moja hadi lingine. Aidha, *Kenya Demographic Heath Survey* (1998) yaonyesha kuwa tohara kwa wanawake imepungua katika kabila la Waluhya, lakini kati ya wanawake wa Abagusii, kiwango ni cha kutisha, kwani ni Asilimia 97 ya wanawake walio na umri kati ya miaka 15-19.

Abagusii ni Wabantu wanaopatikana Kusini-Magharibi mwa Kenya. Wamesheheni wilaya nane za utawala: Nyamira, Kisii ya Kati, Gucha, Kisii Kusini, Masaba, Borabu, Gucha Kusini na Manga katika mkoa wa Nyanza. Lugha waizungumzayo ni Ekegusii.

Abagusii wana imani za kitamaduni ambazo wamezishikilia ili kuwatambulisha kama jamii moja. Mila na tamaduni hizo zilijumuisha mahala kuanzia kuzaliwa, tohara, ndoa, utu uzima hadi kifo asema Nyamwaka (2006:25).

Lugha ya Abagusii inatambua hatua za ukuaji wa binadamu na mabadiliko. *Omwana* (mtoto) ni jina lililopewa mtoto asiyezidi miaka kumi. *Omoisia* (mvulana ambaye hajatahiri) au *egesagane* (msichana ambaye hajatahiri). *Omomura* au *omoiseke* (mvulana au msichana aliye tayari kwa ndoa) - pia waliitwa *abasae* (vijana); *omogaka* au *omong'ina* (mwanaume au mwanamke aliye na watoto).

Ingawa baadhi ya sherehe za watoto zimepuuzwa na jamii hii, tohara bado wameishikilia. Tohara kwa wavulana na ukeketaji kwa wasichana katika jamii hii unafanywa kati ya umri wa miaka 15-20. Kila msichana na mvulana alingojea siku hii kwa hamu kubwa. Jamii iliwaandaa kisaikolojia na kwa njia zingine zote. Ukeketaji na tohara ulikuwa daraja la kuvukia hadi utu uzima, uume au uke.

Hatua ya kwanza katika shughuli ya kuwaandaa wasichana kwa ukeketaji ulikuwa ni maandalizi ya awali kabla ya siku ya hafla yenyewe kama vile kuandaa kuni za kutosha, kufahamisha majirani na marafiki na kumtafuta *omosari.*

Halafu, msichana alitengwa kwa muda mfupi ili apewe mafunzo ya kumshajiisha kwa mujibu wa sherehe hiyo. Aliyeonekana mwoga angeachwa. Mafunzo hayo yalisheheni kumfanya aliyetazamiwa kutahiri atembee mwendo mrefu usiku ili kumfanya awe mstahamilivu na jasiri na kumlalisha nyasini akiwa uchi ili kufanya mwili ugande kwa ajili ya upasuaji na kadhalika. Haya yalimwandaa mtahiriwa awe na ujasiri katika kukabili ukeketaji. Aidha, walifunzwa

waliyotarajiwa kufanya baada ya tohara, vile watahusiana na wengine katika jamii na majukumu yao mapya katika jamii.

Ukeketaji unafanywa kwa kukata sehemu ya mbele ya kinembe kwa hatua tatu kulingana na Mokaya (2001:35). Baadaye, msichana alitengwa kwa muhula wa wiki tano hivi. Huu ulikuwa muhula wa kupona na kufunzwa. Hakutakiwa kuonwa na babake au ami yake.

Hatimaye, mtahiriwa alifuzu baada ya kutengwa, ambapo msichana alipewa zawadi na kubarikiwa na wazazi. Wakati huu mtahiriwa alichukuliwa mtoni aoge na nyimbo za kusheherekea hadhi mpya ya *omware* ziliimbwa. Baada ya kufuzu wanakuwa watu wapya wenye majukumu mapya. Baba hakutarajiwa kumchapa msichana aliyetahiriwa. Sasa wamepoteza utoto na wamevaa utu uzima tayari kwa kushiriki ngono, kuolewa na kukuza familia ili kuendeleza kizazi cha jamii ya Abagusii.

Ni katika msingi huu ambapo utafiti huu ulishughulikia ukeketaji wa wanawake katika jamii ya Abagusii wa nchini Kenya. Hii ni kwa sababu ukeketaji wa wanawake umegunduliwa kuwa na madhara mengi kuliko faida. Hivi kwamba jamii nyingi zimeamua kuiacha desturi hii lakini jamii ya Abagusii bado wanaishikilia. Utafiti huu umefafanua lugha inayotumiwa katika shughuli hii na inavyoathiri mielekeo ya wanawake na watu wengine, hali ambayo huendeleza asasi hii. Uchanganuzi wa lugha umefanywa kuhusiana na asasi hii kwa sababu lugha huhusiana na uwezo.Lugha hufafanua itikadi. Na itikadi zinahusiana na lugha kwa sababu matumizi ya lugha ndiyo njia ya kawaida ya kudhihirisha tabia na mienendo ya jamii ambazo kwazo mawazo ya kawaida hutegemea. Isitoshe, uwezo katika jamii ya kisasa huonyeshwa kupitia utendakazi wa lugha kiitikadi. Aidha, itikadi ndiyo njia kuu ya kuunda ukubalifu au upinzani wa dhana yoyote. Kwa hivyo, utafiti huu umeangazia vile lugha inayotumiwa inavyobainisha utambulisho wa kijamii na mahusiano ya kijamii. Aidha, usemi katika nyimbo za tohara unachanganuliwa ili kudhihirisha athari ya lugha katika usemi huu inayoelekea kuzua na kudumisha itikadi hii ya kukeketa wanawake ilhali ina madhara mengi.

### 1.2 Suala la Utafiti

Licha ya kampeni za kitaifa na za kimataifa dhidi ya ukeketaji, asasi hii haijaachwa bado. Utafiti huu ulichunguza jinsi lugha inayotumika katika usemi wa ukeketaji inavyokuza asasi hii.

### 1.3 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu ulidhamiria kutimiza malengo yafuatayo:

a) Kufafanua sifa za lugha inayotumiwa katika usemi wa ukeketaji.

b) Kutathmini vile utambulisho wa kijamii na mahusiano ya jamii yanavyojengwa kupitia usemi huu.

c) Kudhihirisha athari za lugha inayotumiwa katika kuendeleza ukeketaji.

### 1.4 Nadharia Tete

a) Lugha inayotumiwa katika usemi wa ukeketaji ina sifa mahususi.

b) Asasi ya ukeketaji wa wanawake hujenga utambulisho wa kijamii na mahusiano ambayo hudhihirika katika usemi unayoizunguka.

c) Lugha inayotumiwa katika usemi wa ukeketaji huendeleza ukeketaji.

### 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika uchunguzi wa kiisimu wa ukeketaji wa wanawake katika juhudi za kufafanua sifa za lugha inayotumiwa katika usemi huu, jinsi inavyojenga utambulisho wa jamii na athari yake katika asasi hii. Hii ni kwa sababu matumizi ya lugha ndiyo njia ya kawaida ya kudhihirisha tabia na mienendo ya kijamii ambazo kwazo mawazo ya kawaida hutegemea. Hivyo, uchunguzi wa lugha inayotumiwa katika usemi wa ukeketaji imetupa picha halisi ya chanzo cha asasi hii ya ukeketaji.

Matokeo ya utafiti yatakuwa ya manufaa kwa wasomi wa Fasihi Simulizi na wote wanaojihusisha na kampeni dhidi ya ukeketaji wa wanawake. Aidha, utawanufaisha wasomi wanaotafiti kwa kutumia nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi na maswala ya kiuana.

### 1.6 Upeo na Mipaka

Utafiti uliangazia usemi wa ukeketaji ambao unaegemea katika kuendeleza asasi hii. Aidha, ulizingatia vile usemi wa matini unavyojenga utambulisho wa kijamii. Isitoshe, sifa mahususi za lugha ya usemi huu zilidhihirishwa.

Lugha iliyotumiwa ilichanganuliwa kwa kuangazia nomino, vivumishi, takriri, jazanda na maudhui katika usemi wa ukeketaji ili kufasili na kubaini imani na maingiliano yanayosheheni

usemi huu na mchango wao katika asasi hii. Utafiti ulimulikia ukeketaji katika jamii ya Abagusii wa nchini Kenya.

## SURA YA PILI

## MAPITIO YA MAANDISHI

### 2.1 Utangulizi

Sura hii imeangazia tafiti mbalimbali zilizofanywa na maandiko mbalimbali yaliyopitiwa, yanayohusiana na ukeketaji wa wanawake katika jamii ya Abagusii. Aidha, tafiti zilizofanywa kwa kuzingatia uchanganuzi wa usemi hasa Uchanganuzi Hakiki Usemi zimepitiwa. Mtafiti ameangazia uhusiano kati ya lugha na uwezo hasa akiegemea katika muktadha wa ukeketaji. Isitoshe, nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi na ufaafu wake katika kuongoza uchanganuzi wa deta iliyochanganuliwa imeangaziwa.

### 2.2 Ukeketaji wa Wanawake

Ukeketaji wa wanawake ni kuondoa sehemu fulani za siri za wanawake. Ukeketaji hujihusisha na kukata kinembe au kukata sehemu zingine za uke na hata kushona sehemu ya uke wakiacha tundu ndogo la kutolea mkojo. Jamii mbalimbali ambazo huenzi asasi hii hutumia njia mbalimbali za ukeketaji lakini njia yoyote ile ni hatari. Hakuna njia bora ya kukeketa iwapo inaathiri kinembe au sehemu za uzao za wanawake.

Ukeketaji wa wanawake ni mojawapo ya shughuli inayowaandaa wasichana kuingia katika utu uzima, ingawa umri ambapo inatekelezwa hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Kulingana na Toubia (1993:9) wasichana wengi hukeketwa katika umri wa kati ya miaka minne na minane, wakati wanapewa majukumu ya kijamii wanayotarajiwa kutekeleza.

Jamii zinazoenzi asasi hii huuita tohara ya wanawake. Istilahi hii hata hivyo hulinganisha tohara ya wanaume isiyokeketa na hii ya wanawake ambayo, hasa ni ukeketaji. Tohara ya wanaume huhusisha kukatwa kwa ngozi kutoka kwa kilele cha dhakari. Njia ya ukeketaji inayofuatwa hutegemea umri, jamii anamotoka, nchi yake anamoishi (mjini au mashambani) na tabaka la wasichana.

Jamii nyingi hukeketa katika umri kati ya miaka minne na minane. Kulingana na WHO (1997:20) umri wa kukeketwa unaendelea kupungua. Hii inamaanisha shughuli hii inaendelea kupunguza uhusiano wake na kule kuendeleza utu uzima hasa mijini.

Wasichana wengine hukeketwa peke yao lakini wengine hukeketwa katika makundi, kwa mfano dada, majirani, binamu au wasichana wa umri fulani. Ukeketwaji huweza kufanywa nyumbani kwa msichana au kwa jirani, hospitali ama katika mahali teule kama vile chini ya mti

fulani au mto. Wasichana wanaokeketwa wana ufahamu tofauti kuhusu kinachowafanyikia. Wakati mwingine huwa kuna sherehe na zawadi zinazohusishwa na shughuli hii. Wasichana hujasirishwa kukubali kukeketwa ili wavuke hadi utu uzima. Sherehe za kukeketwa huwa za kufana katika jamii zinazoenzi shughuli hii. Wanawake ndio pekee huruhusiwa kuwa katika sherehe hii. Wanaume huwa kama hadhira tu.

### 2.3 Msambao wa Kijiografia wa Ukeketaji


Toubia (1993:5) atueleza kuwa kila mwaka wasichana takribani milioni mbili wamo katika athari ya kukeketwa ulimwenguni – elfu sita kila siku. Takribani milioni 114 ya wasichana na wanawake ulimwenguni wameketwa. Wengi wa hao wanaishi Afrika, wachache katika bara la Asia na wengine wanazidi kuongezeka katika bara la Uropa, Kanada na Marekani.

Nayo *Human Rights Information Pack* (1997:2) yadhihirisha kuwa takribani milioni 135 ya wasichana na wanawake wamekeketwa ulimwenguni. Hakuna hesabu halisi ya kuonyesha ilivyosambaa bara Asia. Aidha, ukeketaji umeripotiwa miongoni mwa waislamu waishio Indonesia, Sri Lanka na Malasia ingawa ni machache yahusuyo ukeketaji katika nchi hizi yanayojulikana. Nchini India, kikundi kidogo cha waislamu, *Daudi Bohra*, hukeketa wanawake kwa kukata kinembe. Katika Mashariki ya Kati, ukeketaji wa wanawake hupatikana Oman, Yemen na Milki ya Falme za Kiarabu. Aidha, ripoti kuhusu ukeketaji zimepatikana kati ya wakazi wa Marekani ya Kusini na Kati ingawa ni machache yanayojulikana. Katika mataifa yaliyoendelea, ukeketaji unasikika sana kati ya waliohamia kutoka nchi zilizo na mila hii. Umeripotiwa Australia, Kanada, Denmark, Ufaransa, Italia, Uholanzi, Uswisi, Uingereza na Marekani. Hakuna idadi halisi ya wahasiriwa imetolewa katika nchi hizi.

Isitoshe, Mokaya (2001:26) asema kuwa kati ya mataifa hamsini ya Afrika, ishirini na saba huendeleza ukeketaji wa wanawake yaani asilimia 54. Nchi zilizo na asilimia chini ya 50 ni Uganda, Zaire, Tanzania, Senegal, Niger, Kameruni, Mauritania na Ghana.

Mataifa yaliyo na kiwango kati ya asilimia 51-70 ni Chadi, Cote d'Ivore, Liberia, Nigeria na Burkina Faso inavyodhihirika katika jedwali lifuatalo:


**Grafu 1: Nchi zilizo na asilimia kati ya 51-70**




ASILI: Mokaya (2001:26)

Mataifa yaliyo na kiwango cha juu zaidi cha ukeketaji ni Djibouti, Ethiopia, Eritrea, Mali, Sierra Leone, Somalia na Sudan inavyodhihirika katika jedwali lifuatalo:

**Grafu 2: Nchi zilizo na asilimia zaidi ya 70**




ASILI: Mokaya (2001:27)

Nchini Kenya zaidi ya asilimia 50 ya wanawake wamekeketwa. Haya ni madai ya Mokaya (2001:26) na Toubia (1993:25). Kwake Toubia, Wakenya wanawake takribani milioni 6.3 wamekeketwa. Hali hii inaendelea kudidimia mijini lakini inaendelea kuimarika vijijini hasa katika mkoa wa Bonde la Ufa.

Mokaya (2001:24) adai kuwa tafiti za maendeleo ya wanawake na *Programme for Appropriate Technology in Health* (*PATH*) nchini Kenya zinadhihirisha kuwa takribani makabila 30 kati ya 42 huendeleza ukeketaji. Miaka ya kutahiri hubadilika kutoka kabila moja hadi lingine. Aidha, *Kenya Demographic Health Survey ya 1998* yaonyesha kuwa tohara kwa wanawake imepungua katika kabila la Waluhya, lakini kati ya wanawake wa Abagusii, kiwango ni cha kutisha, kwani ni asilimia 97 kwa wanawake walio na umri kati ya miaka 15-19. Isitoshe, makabila ya Mijikenda na mengine ya Waswahili desturi hii ilienziwa katika viwango vya chini kabisa.

Hali hii inadhihirisha vile ukeketaji ulivyoshika mizizi miongoni mwa Abagusii na yahitaji mikakati mwafaka ya kukabiliana nao. Mila hii imeshikiliwa na wengi licha ya kampeni kabambe za kutaka itupiliwe mbali. Ndiposa utafiti wetu umeangazia jamii hii ili kuchunguza athari ya lugha katika kuendeleza mila hii.

## 2.4 Madhara ya Ukeketaji Wanawake

Kuna madhara mbalimbali yanayotokana na ukeketaji:Ukeketaji unaweza kusababisha kifo kutokana na mshtuko kwa kutokwa na damu nyingi. Utafiti uliofanywa na Shirika la Afya Ulimwenguni mnamo Juni 2007 kwa wanawake 28,393 unadhihirisha kuwa aina zote za tohara ya wanawake huathiri mama anapojifungua kwani asilimia 30 hupasuliwa. Pia utafiti huu unadhihirisha kuwa takriban watoto 10-20 kwa 1000 barani Afrika hufa wakati wa kujifungua kutokana na mama kutahiriwa. Aidha, wakati wa kukeketwa kuna kuhisi maumivu makali, kuzirai, kutokwa na damu nyingi na uharibifu wa sehemu za uke kama vile kinembe. Kulingana na uchunguzi wa PATH wa 1991 ambapo wanawake 1,222 kutoka wilaya nne nchini Kenya walihojiwa ilidhihirika kuwa asilimia 48.5 ya wanawake walitokwa na damu nyingi,asilimia 23.9 waliambukizwa maradhi tofauti na asilimia 19.4 walipatwa na kukwama kwa mkojo. Madhara mengine ya kudumu ni kuharibika kwa mishipa ya kupitisha mkojo, kuharibika kwa figo, mishipa ya uzaaji na hata utasa.

Ensaikropedia Wikipedia yadhihirisha kwamba utafiti uliofanywa umethibitisha kuwa uwezekano wa kupata virusi vya HIV huongezeka kwa wanawake waliotahiri. Ikimtaja Kanki et al (1992), inasema kuwa kule Senegal makahaba waliotahiri hawakuwa na hatari ya kupata virusi vya HIV ukilinganisha na wale ambao hawajatahiri. Kwingineko, inadhihirisha kuwa wanawake waliotahiri hawakuwa katika hatari ya kuambukizwa virusi ilhali ambao hawakutahiri walikuwa na hatari maradufu ya kuambukizwa virusi nchini Tanzania.

Wakati mwingine kujamiiana kwa mara ya kwanza kunakuwa kugumu na kwenye maumivu makali kwa aliyekeketwa. Ukeketaji hufanya kushiriki ngono kuwa jambo la kuudhi na maumivu kwa wanawake. Isitoshe, ngono hairidhishi matakwa ya mwanamke kwani kinembe ambacho huleta furaha na kuridhika kimekatwa kutokana na ukeketaji. Kwa hivyo, kujamiiana hakumletei mwanamke kuridhika inavyokuwa kwa mwanamume ambaye sehemu zake za kuridhika kingono hazijakeketwa. Hata hivyo utafiti uliofanywa nchini Sudan ulidhihirisha kuwa asilimia 90 ya wanawake waliohojiwa walikiri kuwa wao hufurahia ngono hata kama wametahiri. Kwa hivyo hawaoni ubaya wa tohara ya wasichana.

Madhara ya kisaikolojia ya ukeketaji huwa vigumu kuchunguza kisayansi, hata hivyo ni visa vichache vya athari za kisaikolojia viliripotiwa. Hali ya shauku, kusalitika na woga hukumba waliokeketwa ambayo huathiri mwanamke kisaikolojia. Katika utafiti uliofanywa na Pharos mnamo Februari, 2010 pale Uholanzi ilidhihirika kuwa wanawake waliotahiri huathirika kisaikolojia. Katika utafiti huu wanawake asilimia 66 ya wale waliohojiwa walipatikana na usumbufu wa akili kutokana na kupitia asasi ya tohara.

Athari ya kisaikolojia ambayo imemfaidi aliyekeketwa ni kule kuhisi kubadilika katika jamii, kwa kufuata imani za utamaduni wake na kujifanya aweze kuolewa. Kwa hivyo inawezekana yule ambaye hajatahiri awe na madhara ya kisaikolojia kwa kutokubalika katika jamii yake. Kulingana na Mbugua (1997:19) msichana ambaye alikaidi tohara hutengwa na kufukuzwa na wazazi. Hali pia ingemwathiri kisaikolojia msichana husika kwa kutokubalika na wazazi na jamii kwa ujumla.

Nalo gazeti la *Daily Nation* ya Ijumaa, Juni 30, 2006, ladhirisha kuwa ukeketaji wa wanawake ndio mojawapo ya mila hasi ambayo imekuwa changamoto kubwa katika harakati za kuendeleza elimu. Hii ni kwa sababu inawafanya vijana wengi aghalabu wasichana kuacha shule na kushiriki ndoa za mapema. Akijenga wazo lili hili Mbugua (1997:19) asema kuwa uja uzito miongoni mwa wasichana waliotahiri huongezeka. Hata anadai walimu wamethibitisha kuwa

matokeo ya mtihani kwa wale waliotahiri hudidimia. Hali hii imedhihirika katika sehemu kadhaa nchini Kenya kama vile wilaya ya Kuria na sehemu nyingi za mkoa wa Bonde la Ufa.

## 2.5 Sababu za Kuenzi Ukeketaji wa Wanawake

Kuna sababu nyingi zinazochangia kuenzi ukeketaji wa wanawake: Kupata utambulisho wa kitamaduni. Mila na itikadi ndizo sababu zinazotajwa zaidi ambazo huwachochea wengi kukeketwa. Hii ni kwa sababu ukeketaji ni njia mojawapo ya kutangaza aliye wa jamii na asiye. Kenyatta (1938:21) adai kuwa ukeketaji ni wa muhimu katika kukua na kuvuka daraja kutoka utotoni hadi utu uzima na hivyo ni sehemu muhimu ya kuwa *Mkikuyu*, kwa hivyo kuikataa kutaharibu mifumo ya kabila hili.

Madai haya yanaenziwa na jamii nyingi zinazoshikilia mila hii. Wanadai kuwa msichana aliyepuuza tohara ameasi jamii na hivyo jamii husika ilimbagua kama asiye wao. Watu wengi katika jamii zinazoenzi mila hii huuona ukeketaji kama jambo la kawaida hivi kwamba hawafikirii uwezekano wa yeyote kuiasi. Wengine hata husema ni wageni au wasio wa jamii ndio watapuuza mila hii.

Aidha, wengi huenzi ukeketaji ili kupata utambulisho wa kiuana. Kwa jamii nyingi ukeketaji ni muhimu kwa msichana ili aweze kuhesabiwa mwanamke kamili na asasi hii hudhihirisha tofauti za majukumu kwa kila jinsia. Kukatwa kwa kinembe kilichochukuliwa kama sehemu ya mwili wa mwanamume katika mwili wa mwanamke huendeleza uke wa msichana na huchukuliwa kuwa utiiifu. Naye Nyang'era (1999:36) adai kuwa ukeketaji ulimfanya msichana aweze kujiandaa kwa majukumu ya umama na uke katika maisha ya ndoa. Hii ni kwa sababu ukeketaji uliambatana na mafunzo kuhusu majukumu ya mke katika jamii husika.

Katika jamii nyingi, sababu kuu ya kukeketa wanawake ni imani kuwa kunapunguza ashiki ya wanawake na hivyo kupunguza ngono nje ya ndoa. Kulingana na *Human Rights Information Pack* (2006:5) uwezo wa wanawake ambao hawajakeketwa kuwa waaminifu katika ndoa kwa uteuzi wao hauaminiki. Njia ya pekee ya kumzuia mwanamke asishiriki usinzi ni kumkeketa. Akizuiwa kwa njia hii, heshima kwa familia ya msichana huyo itakuwepo kwani hatauharibu kwa kushiriki usinzi. Hata hivyo, madai haya hayana mashiko kwani imedhihirika wazi kuwa hata wanawake waliokeketwa hushiriki usinzi na uasherati.

Wengi huamini kuwa aliyekeketwa huwa safi ukeni asemavyo Toubia (1993:37). Kwa hivyo, katika jamii zinazoenzi mila hii mwanamke ambaye hajatahiri huchukuliwa kuwa mchafu na hivyo haruhusiwi kugusa chakula na maji ya kutumika kwa vyakula. Sehemu za uke za wale ambao hawajatahiri huchukuliwa kuwa nzito na zisizo na sura. Wengi hata huamini kinembe ambacho hakijakatwa kikigusa dhakari ya mwanamume atakufa. Aidha, wengine huamini kuwa kichwa cha mtoto anayezaliwa kikigusa kinembe, mtoto anaweza kufa. Imani hizi hufanya wengi kuhitaji kukeketwa. Hata hivyo, hizi ni imani zisizo na mashiko.

Isitoshe, Toubia (1993:37) amesema kuwa jamii nyingi huamini kuwa Mungu ametakasa ukeketaji. Biblia haijazungumzia swala la ukeketaji wa wanawake lakini wahubiri na washiriki wengine hawajajitokeza wazi kuilaani bali wameivumilia katika kanisa. Hata hivyo, kuna wahubiri wengine wameikemea na hata kutafuta njia badala ya kuvusha wasichana kutoka utotoni hadi utu uzima. Hata hivyo, tohara ya wavulana imekubaliwa na kuenziwa katika Biblia. Katika dini ya Kiislamu baadhi ya wafuasi wameishikilia mila hii wakidai dini hii imeikubalia. Lakini Korani na mafunzo ya Mtume Mohammed hayajazungumzia swala hili. Kwa hivyo, madai kuwa dini yoyote inaruhusu ukeketaji wa wanawake ni uongo mtupu.

Kulingana na Castledine (2010:2) watu wengine hushikilia asasi hii ya ukeketaji kwa sababu ya manufaa ya kiuchumi. Anadai kuwa kwa wasichana wanatamani kutahiri ili wapate zawadi kutoka kwa watu wa familia zao na pia wapate heshima kutoka kwa wenzao na jamii kwa ujumla. Aidha, anayetahiri huoleka kwa urahisi hivyo wazazi hupata mahari nyingi na kwa haraka.Hivyo kila mzazi angetamani kumtahiri msichana wake ili apate mahari. Isitoshe, wale watahiri pia hulipwa vizuri na kupewa zawadi baada ya kutekeleza wajibu. Pia walipewa heshima kubwa kwa huduma yao. Hali hizi za matarajio ya kufaidi kiuchumi kwa makundi mbalimbali ya jamii ilipelekea kila mmoja kutamani kuendeleza asasi hii.

## 2.6 Ufafanuzi wa Hatua za Ukeketaji wa Wanawake katika Jamii ya Abagusii

Kulingana na Mokaya (2001:28) Abagusii walithamini uke na uume kama chanzo cha maisha. Tohara ilikusudiwa kufungua sehemu hizo ili kuhakikisha kuendelea kwa maisha kupitia kuzaa. Kila mwanamke alistahili kukeketwa kabla ya ndoa. Baada ya tohara, wasichana waliolewa, waliruhusiwa kushiriki mapenzi na kupata watoto.

Mwanamke yeyote aliyekosa kutahiriwa au aliyeasi mila yoyote ya tohara alihesabiwa msaliti wa pepo za mababu na jamii yote ya Abagusii. Waasi kama hao wangeadhibiwa au

wangeolewa kwa njia duni, kama vile, mahari ingelipwa ndogo, angeolewa na mzee, kilema au mtu wa tabaka la chini. Aidha, iliaminika mwanamke ambaye hajatahiri angepata watoto waliokufa kabla ya umri wa makamo au hawawapati mabwana wazuri au kinembe kingekua kiwe kirefu kiasi cha kutomuwezesha kushiriki ngono.

Itikadi na imani hizi ziliwatisha wasichana na hivyo kuogopa kutotahiriwa. Damu iliyomwagika wakati wa tohara ilimuunganisha mtahiriwa na mababu wa Abagusii. *Obware* ilihusisha hatua nne: Maandalizi ya watahiriwa, tohara yenyewe, kutengwa kwa watahiriwa na sherehe ya kufuzu.

### 2.6.1 Maandalizi ya Watahiriwa

Maandalizi ya *obware* yalichukua miezi mingi kabla ya msimu wa mavuno kila mwaka. Shughuli za *obware* zilifanywa kati ya mwezi wa Agosti na Disemba. Watahiriwa walio na umri wa miaka kumi na zaidi walitarajiwa kujiandaa kihisia, kisaikolojia na kimwili. Kuni za kutosha zilikusanywa, ambazo zingetumiwa kuhifadhi moto wa sherehe hii wakati wa kutengwa ambao ni takribani wiki tano. Kuni hizo zingekuwa za miti migumu ambayo haizimiki kwa urahisi. Miti hiyo ni pamoja na *omokonge, omotamaywa, omobera, omonyenya, omoraa, ekieyo, omosabakwa, omwobo* na *emete ememwamu.*

Pia maandalizi yalihusisha ujenzi wa *egesa* kwa matumizi ya baba wa mtahiriwa huku yeye akiachwa na mamake kwa nyumba kuu. Isitoshe, vyakula vya kutosha vilitafutwa kwa mujibu wa sherehe hiyo. Majirani na masahibu walifahamishwa ili kujiandaa kwa sherehe na pia kutoa zawadi (*egetoro*) kwa mujibu wa sherehe hizo. Siku kabla *egesagane* hajatahiri, wanawake wengi walialikwa kwa nyumba ya mtahiriwa kama sehemu ya maandalizi. *Omosari* pia alitafutwa mapema ili ajulikane atakapopatikana siku ya tohara kwani walikuwa wachache.

### 2.6.2 Kukeketwa

*Egesagane* alitahiriwa baada ya kunyolewa nywele zote kichwani, wasichana walio mahiri hualikwa kumchukua mahali pa tohara yenyewe, vyakula vya kutosha kuandaliwa na *omosegi* kutambuliwa na wazazi wa mtahiriwa. Nywele za *egesagane* zilinyolewa kama ishara ya maandalizi halisi kwa tohara yenyewe na mwanzo mpya kwa mtahiriwa. Alihimizwa asilie, kupiga kelele au kumshika *omosari.*

*Ebisagane* wote waliokuwa tayari kwa tohara walitembea kwa baridi wakiwa uchi na kuoga maji baridi asubuhi kabla ya machweo ili kuleta ukosefu wa hisi wakati wa kutahiriwa. Wakati wa kutahiriwa , *egesagane* alikalishwa kwa jiwe au ngozi ya mbuzi. Mtahiri alitumia kisu, mfuko wa ngozi, ngozi ya mbuzi na jiwe la kutia makali. *Omosari* alihifadhi hivi vifaa vyake na kuvitumia kila mara hadi kifo chake au atakaposhindwa kuona. Mtahiriwa hushikwa na wanawake wawili , halafu *omosari* humnyunyizia unga wa wimbi kwa kinembe chake kisha kukata sehemu ya mbele ya kinembe chake kwa hatua tatu. Ni kisu kimoja tu kilitumika kukata wateja wote waliohudhuria siku husika. *Enkuri* ( aliyelia wakati wa tohara) angedunishwa na wasichana wengine katika maisha yake yote, hata jamii nzima.

Baada ya kutahiriwa, watahiriwa wote waliwekwa foleni kwa utaratibu waliotahiriwa kisha *omosari* anapewa zawadi za mazao na kiongozi wa kila *egesagane*. Halafu, kila mtahiriwa alipewa mimea iitwayo *ebirundu* ambayo ilihifadhiwa hadi kufuzu. Baadaye, *omosari* angeanzisha *esimbore* (wimbo wa tohara) halafu wanawake waliohudhuria waliimba wakirudi makwao. Kuanzia hapa, mtahiriwa angebadilisha jina kutoka *egesagane* hadi *omware* hadi siku ya kufuzu atakapoitwa *omoiseke* au *enyaroka.*

### 2.6.3 Muhula wa Kutengwa

Muhula wa kutengwa ulichukua kati ya wiki tano hadi kumi. Huu ulikuwa muhula wa kupona na kupata mafunzo mbalimbali yahusuyo uzazi, maadili na utamaduni wa jamii. *Omware* hakutakiwa kuonwa na babake au ami wake. Baada ya kufika nyumbani, moto wa sherehe uliwashwa na nyanyake mtahiriwa, na ulihifadhiwa hadi siku ya mahafali. Iliaminika kuwa ikiwa moto ungezimika, hiyo ni bahati mbaya na laana kwa *omware* na *omosegi*. Wakati wa kutengwa, *omware* alitarajiwa kuulinda moto usizimike, asioge mwili bali aupake majivu, asionwe na watu, azungumze kwa sauti ndogo ili asisikike na watu na anyunyizie maji *esuguta.*

### 2.6.4 Kufuzu

Hii ni sherehe ya kutoa mtahiriwa jandoni baada ya kutengwa kwa muda wa zaidi ya wiki tano. Sherehe hii ilihusisha wasichana wachache, *omware*, watu wa familia yake na wazazi. Ilikuwa wakati wa kupata baraka na kupokea zawadi. Wakati huu *esuguta* iling'olewa, *omware* alichukuliwa mtoni aoge na nyimbo za kusherehekea hadhi mpya ya *omware* ziliimbwa.

Mwili wa *omware* ulipakwa udongo uliochanganywa na mafuta (*engenyi*) na alivaa nguo mpya. Halafu alibadilisha hadhi kutoka *omware* hadi *omoiseke*. Mimea ya *amabuko* ilichomwa kama ishara ya kuonyesha kutoweka kwa utoto kabisa na kuingia kwa utu uzima.

Baada ya kufuzu, wanarudi kwa jamii kama watu wapya wenye majukumu mapya. Baba hakutarajiwa kumchapa msichana aliyetahiriwa. Sasa wamepoteza utoto na wamevaa utu uzima, tayari kwa kuolewa, kushiriki mapenzi na kukuza familia ili kuendeleza kizazi cha jamii ya Abagusii.

## 2.7 Tafiti Zinazohusiana na Ukeketaji

Ingawa upeo kamili wa msambao wa ukeketaji nchini Kenya haujapatikana, Nyansera asema kuwa asilimia 85 za jamii nchini Kenya hushiriki desturi hii ilhali asilimia 15 yazo wakiwemoWajaluo na Waturkana, hawashiriki desturi hii. Akiangazia jamii ya Abagusii Nyansera aeleza hatua nne za kuvuka maishani yaani: Kuzaliwa na sherehe zake, ndoa, mazishi, na tohara. Asema kuwa hatua tatu za mwanzo zimeanza kufifia lakini desturi ya tohara inaendelea hadi leo (1994:1). Adai, hii ni kwa sababu ya jukumu kubwa la tohara katika ujumuishaji na utangamano wa wanajamii ya Abagusii. Utafiti wa Nyansera ulishirikisha wahojiwa 200 wa kike. Kutokana na mahojiano hayo ametoa jedwali lifuatalo linaloakisi jinsi ukeketaji ulivyotamalaki jamii ya Abagusii (1994:39). Deta yake inalinganisha kati ya wanawake waishio mijini na wale wa mashambani na ikiwa wanajua madhara ya ukeketaji na kama wataruhusu wasichana wao kuushiriki.

**Jedwali 2: Msambao wa Ukeketaji Katika Wilaya ya Kisii**

| | Mashambani | | | | Mjini | | | | Jumla | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Majibu** | **Ndio** | **%** | **La** | **%** | **Ndio** | **%** | **La** | **%** | **Ndio** | **%** | **La** | **%** |
| **Wajua Ukeketaji** | 98 | 98 | 2 | 1.0 | 99 | 99 | 1 | 0.5 | 197 | 98.5 | 23 | 1.5 |
| **Wamekeketwa** | 98 | 98 | 2 | 1.0 | 95 | 95 | 5 | 5.0 | 193 | 96.5 | 7 | 3.5 |
| **Watoto wao wamekeketwa** | 87 | 87 | 13 | 13 | 78 | 78 | 22 | 22 | 137 | 68.5 | 63 | 31.5 |

ASILI: Nyansera (1994:39)

Kutokana na jedwali hili, ni wazi kuwa ukeketaji umesambaa sana ambapo asilimia 95 ya wahojiwa wamekeketwa. Hata wale wa mjini hawajaachwa nje katika shughuli hii. Ndiyo maana Nyansera asema kuwa ukeketaji waendelea "bila kujali imani za kidini za watu, kiwango cha elimu na aina ya kazi wafanyazo" (1994:49). Cha kushangaza zaidi kutokana na jedwali hili ni ukweli kuwa asilimia 68 ya wahojiwa wanasema watakeketa wasichana wao. Hii ni baada ya kukubali ukweli kuwa wanajua madhara ya shughuli hii. Nyansera adai kuwa vifo 70 kati ya 1000 katika jamii huletwa na madhara ya ukeketaji. Hiki ni kichocheo cha utafiti wetu, kutaka kujua lugha ina mchango gani katika kukuza desturi hii ikiwa wanajamii ya Abagusii wamejua madhara ya shughuli hii na bado wangali wanaikuza.

Mtafiti mwingine ambaye amemulikia mada hii ya ukeketaji ni msomi Ali, A.M. Ali ameangazia sababu za kijamii na kitamaduni zinazoendeleza ukeketaji miongoni mwa Wasomali ambao ni Waislamu. Utafiti wake umedokeza sababu kama vile: dini, ndoa, utambulisho wa jamii na mafunzo ya maadili miongoni mwa sababu zingine kama vichocheo vya kuendeleza mila hii. Utafiti wake umeonyesha kuwa, ingawa watu wa jamii hii wanaelewa madhara ya desturi hii bado wanaendelea kuishikilia. Amependekeza hatua zinazostahili kuchukuliwa ili kuzuia ukeketaji kama vile: sera madhubuti ya serikali, kampeni kali inayoshirikisha wanaume, wahudumu wa afya, wateteaji haki za wanawake na mashirika mbalimbali yasiyo ya serikali. Hata hivyo, mapendekezo yake hayajafuatwa kwani tafiti za baadaye zilizofanywa zaonyesha kuwa asilimia kubwa ya jamii ya Wasomali bado wanashikilia desturi hii. Kwa mfano, utafiti

uliofanywa na UNICEF (2005:6) waonyesha kuwa asilimia 98 ya Wasomali bado hukeketwa.

Vivo hivyo, msomi mwingine Elmi ameangazia ukeketaji katika jamii ya Wasomali.Yeye amemulikia shida za kiafya zinazowapata waliokeketwa katika jamii hiyo. Cha kushangaza pia kutokana na utafiti wa Elmi ni kuwa asilimia 67.6 ya wahojiwa wanatamani wasichana wao wakeketwe hata ingawa wanajua madhara ya kielimu na kiafya yanayokumba waliokeketwa. Wanaamini kuwa bado ukeketaji una manufaa (2003: xii). Elmi adai kuwa kile Wasomali wamekubali ni ukeketaji ambao hauna maumivu sana kama ule wa hapo awali. Huyu mtafiti adai kuwa katika nchi ya Kenya, jamii za Wasomali na Abagusii wanashiriki ukeketaji kwa asilimia kubwa ya 97. Ni katika msingi huu ambapo tumetoa mchango wetu wa kiisimu katika kuchunguza kukua kwa desturi hii kupitia utafiti wetu.

Hatimaye, mtafiti Mose ametoa mchango wake kuhusu mada hii ya ukeketaji. Yeye pia ameangazia jamii ya Abagusii. Yeye, kando na Nyansera amezungumzia jinsi ukeketaji hujumuisha wanawake katika majukumu yao katika jamii ya Abagusii. Mose (1997:64) asema kuwa wanawake wa jamii ya Abagusii waliamini sana kuwa majukumu yao katika jamii yaliamuliwa na Mungu, kwa hivyo hawakuwa na haki ya kulalamikia hali zao. Asema, hili linaeleza kwa nini wametosheka na majukumu na hadhi yao waliyopewa na jamii. Amali zilizotiliwa mkazo katika miviga ya ukeketaji zilikuwa na umuhimu mkubwa kwa kuleta utangamano na kuendelea kwa jamii hii (1997:71). Hata hivyo anasema kuwa mchakato huu wa kupokeza amali za jamii kwa wanajamii ulikuwa na upungufu wake: wapokeaji (wanawake) hawakupewa fursa ya kuulizia maudhui ya mafunzo hayo; mchakato huu ulitumika kunyanyasa sehemu fulani ya jamii. Wanawake walitiwa utumwa na amali walizofunzwa na wale ambao hawakutaka kufuata miviga hiyo walishurutishwa na wale walioipitia hivi kwamba kikundi chote cha wanawake katika jamii kiliathiriwa na ukeketaji kama njia ya kujamiishwa.

Vilevile, Mose asema kuwa utafiti wake ulionyesha kuwa akina mama waliongoza katika uamuzi wa kukeketa wasichana wao ingawa akina baba hawakuachwa nyuma. Adai kuwa, ujamiishaji kupitia ukeketaji uliwapokeza wasichana mafunzo yaliyowaelezea hadhi na majukumu yao katika jamii ambayo waliyaamini na kuyafuata (1997:107). Kwingineko, katika utafiti wake Mose amesema kuwa nyimbo zilidhihirisha furaha katika shughuli hii na pia kudhihirisha mielekeo ambayo watahiriwa walihitajika kuishikilia (1997:48, 49). Hatimaye, Mose amesema kuwa ukeketaji unaendelezwa katika jamii hii ya Abagusii kwa sababu wanaamini ni utamaduni wao kufanya hivyo na ni njia mahususi ya kujitambulisha kijamii.

Wengine hata wanadai ni njia ya kutofautisha wanawake wa Gusii na wale wa Ujaluoni (1997:139).

Tafiti tulizozirejelea kwa ujumla zinaunda msingi imara wa utafiti wetu. Kwanza, tafiti hizo tulizozirejelea zimetumia mikakati ya kisosiolojia ilhali huu wetu umechukua mikakati ya kiisimu katika kubainisha mchango wa lugha katika kuendeleza desturi hii ya ukeketaji. Aidha, tafiti hizo zote zimedhihirsha kuwa jamii ya Abagusii, licha ya kampeni kali, bado ingali inashiriki tohara kwa asilimia kubwa (97%). Utafiti wetu umemulikia jinsi lugha inavyochangia hali hii na jinsi ya kuzuia kukua huku.

## 2.8 Lugha na Uwezo

Uhusiano kati ya lugha na uwezo unaweza kufafanuliwa kupitia dhana ya itikadi. Itikadi ni jinsi mtu anavyouona ulimwengu. Fairclough (1989:2) aeleza itikadi kama mawazo yanayokubalika ambayo hudhihirika katika kaida ambazo kwazo watu hutangamana kiisimu bila wao kujua. Huyu msomi adai kuwa itikadi ina uhusiano wa karibu na uwezo kwa sababu mawazo ya kiitikadi yanayosheheni kaida za usemi hutegemea mahusiano ya kiuwezo ambayo kwayo kaida hizi zimeundwa na mawazo haya huwa msingi wa kuhalalisha mahusiano ya kijamii na tofauti za kiuwezo.

Itikadi zinahusiana na lugha kwa sababu matumizi ya lugha ndiyo njia ya kawaida ya kudhihirisha tabia za kijamii ambazo kwazo mawazo haya ya kawaida hutegemea. Kuonyesha uwezo katika jamii ya kisasa hupatikana kupitia utendakazi wa lugha kiitikadi. Itikadi ndiyo njia kuu ya kuunda ukubalifu wa dhana yoyote.

Wasomi wengine wanasema kuwa matini huwa na maudhui ya kiitikadi. Vestergaard na Shruder wakimtaja Burton (1997:92), wadokeza kuwa itikadi inayopendwa ulimwenguni hupatikana katika ujumbe wa matini, ambazo watu hutumia kila mara na kuzifurahia. Kwa hivyo, nyimbo katika ukeketaji hazijaachwa nje katika mjadala huu, ambazo tumeangazia kama matini za uchanganuzi wetu ili kubaini itikadi zinazojitokeza kiisimu katika usemi wa ukeketaji.

Van Dijk (1997:17) asema kuwa habari za awali na imani huathiri jinsi ya kufasiri matini. Adai kuwa itikadi huunda msingi wa ufasili. Itikadi hupanga mielekeo kuhusu vipengee vya jamii. Van Dijk asema kuwa ni rahisi kudhibiti mielekeo ya mteja ndiposa mteja atatenda ili kufaidi itikadi za mzalishaji. Utafiti wetu umetathmini athari ya itikadi katika nyimbo za ukeketaji katika kuendeleza desturi hii. Lull (1996:7) naye asema kuwa habari za umma hujenga

EGERTON UNIVERSITY LIBRAR

itikadi ambazo huhifadhi mahitaji ya waumbaji. Hii inamaanisha kuwa ujumbe unabeba maoni ya kiitikadi ya wanaoiunda. Takriri ya ujumbe kama huu hutuma dhana ndani ya itikadi za hadhira. Utafiti huu umeshughulikia jinsi nyimbo katika ukeketaji huunda itikadi kwa wanaoupokea na wanavyounda utambulisho wa kijamii kutokana na upokezi huo.

Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi ambayo ndiyo msingi wa utafiti wetu hukubali ukweli kuwa uwezo unaathiri ujenzi wa usemi. Nadharia hii hujihusisha na mahusiano ya kiuwezo miongoni mwa washirika mbalimbali wa jamii. Uhusiano huu umejengeka katika utawala. Kikundi kimoja kimetawala huku kingine kimetawaliwa. Kwa kawaida wenye uwezo hutumia uwezo wao kuwatawala wengine. Nadharia hii humulikia matumizi hayo mabaya ya uwezo na wenye uwezo kupitia kwa kuweka itikadi zao katika usemi. Ndiposa Fairclough (1989:46) anasema kuwa uwezo ndani ya usemi hutokana na washiriki wenye uwezo kudhibiti mchango wa wale washiriki wasio na uwezo. Utafiti huu umedhihirisha jinsi waliotahiri wanavyowatawala ambao hawajatahiri kupitia kwa nyimbo za ukeketaji ambazo wamejaza itikadi zao. Na hali hii inachangia kuendelea kwa asasi hii kwani kushiriki kwa wasio na uwezo (ambao hawajatahiri) kumedhibitiwa na wenye uwezo (waliotahiri).

## 2.9 Msingi wa Nadharia

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi (Critical Discourse Analysis) ambayo hudokeza kuwa usemi na jamii hutegemeana na kujengana. Hii ni nadharia toto ambayo waasisi wake ni Wodak, Fairclough na Van Dijk. Hata hivyo mtazamo na misingi iliyodokezwa na msomi Norman Fairclough (1989, 1992, 1995 na 1996) katika maandishi yake ilikuwa mihimili mikuu ya utafiti wetu.

Kulingana na Fairclough (1992:35) nadharia hii ina mihimili mitano: Kwanza, usemi huundwa na jamii. Ni wazi kuwa matumizi ya lugha huamriwa kijamii na lugha hubadilika kulingana na hali ya jamii inapotumika. Matumizi ya lugha huathiri jamii na vilevile kuundwa nayo. Asasi ya ukeketaji ikiwa mali ya jamii nayo huathiriwa na matumizi ya lugha. Matumizi haya tutayachanganua tukiegemea vile yanavyojitokeza katika nyimbo za tohara ambazo zitaunda matini tutakazochanganua.

Pili, usemi husaidia katika kuunda (na kubadilisha) maarifa, mahusiano ya jamii na utambulisho wa jamii. Tukiegemea mhimili huu tutaweza kuchanganua vile utambulisho wa kijamii na mahusiano ya kijamii yanavyojitokeza katika usemi wa ukeketaji. Katika usemi

wowote, maarifa, mahusiano ya kijamii na utambulisho wa kijamii huundwa au huundwa upya kwa wakati mmoja.

Tatu, usemi huundwa na mahusiano ya kiuwezo na umesheheni imani (itikadi). Mhimili huu hudokeza athari za kijamii katika usemi. Uwezo huathiri kaida za usemi kwa kuzipa imani fulani kwa njia fulani.Hii ndiyo maana katika utafiti huu, usemi wa ukeketaji wa wanawake umewapa uwezo waliotahiri au kutoa imani kwa wale ambao hawajatahiri kufikiria kuwa watapata uwezo zaidi wakishatahiri.

Nne, kuundwa kwa usemi ni swala kuu katika kinyanganyilo cha uwezo/mamlaka. Kwa vile kaida za usemi huathiriwa na jamii kwa njia fulani, basi udhibiti wa michakato ya uzalishaji huwa njia ya wazi ya utawala. Hii ndio njia ambayo kwayo vikundi vyenye uwezo hutawala jamii au nyanja fulani ya jamii. Ndiposa, katika utafiti huu tumeona kuwa kwa vile waliotahiri wamedhibiti uzalishaji wa usemi wa ukeketaji basi wameweza kutawala fikra na imani za wasichana kuwa ukeketaji ndio njia bora ya kupata uwezo/mamlaka.

Mwisho, nadharia hii huonyesha jinsi jamii na usemi hujengana. Katika muktadha huu tumeona vile usemi wa ukeketaji umejenga imani chanya kuhusu ukeketaji hivi kwamba imekuwa vigumu asasi hii kuachwa hata ikiwa ina madhara.


Kwingineko, Fairclough (1996:62) adai kuwa usemi huchangia katika ujenzi wa nyanja zote za muundo wa jamii ambazo huchangia kuziunda au kuzikwamiza kupitia kaida zake, mahusiano, utambulisho pamoja na taasisi zinazosheheni miundo hiyo. Aeleza kuwa usemi ni tendo la kuwakilisha, kuashiria, kuunda na kujenga ulimwengu kimaana.

Anabainisha vipengee vitatu vya kudhihirisha athari za usemi: Kwanza, usemi huchangia ujenzi wa utambulisho wa kijamii. Pili, usemi husaidia katika ujenzi wa mahusiano ya kijamii baina ya watu. Na hatimaye, usemi husaidia katika ujenzi wa mfumo wa maarifa na imani. Haya yalikuwa muhimu kuyachunguza katika utafiti wetu kwani usemi kuhusu ukeketaji uliangaziwa ili kutathmini jinsi usemi huo umechangia katika kujenga mahusiano kati ya waliotahiri na wale ambao hawajatahiri, kuleta utambulisho wa kijamii kati ya washiriki hao na athari ya usemi huu katika ukeketaji.

Isitoshe, vitabu vya Fairclough- *Language and Power* (1989), *Critical Discourse Analysis* (1995) na *Discourse and Social Change* (1996) vimependekeza njia tatu za kufanya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi: Uchanganuzi wa matini; uchanganuzi wa tendo la usemi

(Maingiliano) na uchanganuzi wa tendo la jamii (Muktadha). Njia hizi tatu zimeonyeshwa katika jedwali lifuatalo:

**Mchoro 1: Njia Tatu za Uchanganuzi wa Usemi**




ASILI: Fairclough (1989:25)

Uhusiano kati ya tendo la jamii na matini huoanishwa na tendo la usemi (maingiliano) yaani jinsi matini huzaliwa na kufasiliwa hutegemea tendo la jamii ambalo matini inalihusu; muundo wa matini na sifa zake rasmi na za kimtindo huchunguzwa. Aidha, mchakato wa uzalishaji wa matini hurahisisha ufasili wa matini. Kwa misingi ya jedwali hili nadharia ina sehemu tatu:

i) Kufafanua matini
ii) Kufasili michakato ya maingiliano na mahusiano yao na matini; na
iii) Kueleza vile michakato ya maingiliano inavyohusiana na tendo la jamii.

Sambamba na tanzu tatu za usemi, kuna hatua tatu za kufanya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi:

i) **Ufafanuzi** : Unahusika na sifa rasmi za matini kama vile msamiati, sarufi na miundo ya matini.

ii) **Ufasili:** Unajihusisha na mahusiano kati ya matini na maingiliano (tendo la usemi) hivi kwamba matini huangaziwa kama zao la mchakato wa uzalishaji na kama rasilimali ya mchakato wa ufasili. Katika hatua hii kaida zinazotumiwa hubainishwa na jinsi kaida hizo zilivyotumika huchunguzwa.

iii) **Upambanuzi**: Hujihusisha na uhusiano kati ya maingiliano (tendo la usemi) na tendo la jamii (muktadha wa jamii). Huchunguza sifa za jamii zinazoathiri michakato ya uzalishaji na ufasili na athari zao za kijamii. Hatua ya upambanuzi pia huchunguza mchango wa usemi kwa tendo la jamii, athari za usemi kwa kuunda maarifa, mahusiano na utambulisho wa kijamii. Aidha, hatua hii huangazia athari za kiimani na kisiasa za kaida zilizotumika.

Naye Schiffrin (1987:1) anaunga mkono mtazamo huu kwa kudai kuwa uchanganuzi wa usemi hushughulika na matumizi ya lugha katika miktadha ya jamii. Brown na Yule (1993:1) pia wanaunga mkono mtazamo huu wa Fairclough kwa kusema kuwa uchanganuzi usemi ni uchanganuzi wa lugha katika uamilifu wake. Hivyo basi uchanganuzi huu hauwezi kuwekewa mipaka ya kiisimu bali huhusisha uamilifu wake kwa shughuli za binadamu. Ndiposa utafiti huu umejishughulisha na kuchunguza uamilifu wa lugha katika kukuza ukeketaji wa wanawake.

Msomi Fowler anaonyesha jinsi vifaa vinavyotokana na nadharia wastani za kiisimu za Chomsky ya sarufi na nadharia ya Halliday (utaratibu wa uamilifu wa sarufi). Vifaa hivi vinaweza kutumika kubainisha miundo ya kiisimu ya mamlaka katika usemi wa matini. Fowler (kama hapo juu) anaonyesha jinsi ambavyo utaratibu wa usemi unavyoweza kuasisi, kuendesha na kuhalalisha ngazi za mamlaka katika jamii. Msingi wa nadharia hii ni kuwa lugha yenyewe haina uwezo/mamlaka, bali hupata uwezo huu kutoka kwa wanajamii wenye kumiliki uwezo. Hii ndiyo sababu nadharia ya uchanganuzi hakiki wa usemi huchagua mtazamo wa wale wanaotwezwa na kuchanganua kwa kina matumizi ya lugha ya wale wenye uwezo na mamlaka ambao wamewajibika katika kuendeleza hali ya kutokuwa na usawa katika jamii. Ndiposa katika utafiti wetu tumeangazia nyimbo za tohara ambazo zimeundwa na wenye uwezo (waliotahiri) ambazo zimeakisi matumizi yao ya lugha yanayotetea uwezo wao dhidi ya wale ambao hawajatahiri.

Fairclough na Wodak wanashikilia kuwa lugha ni tendo la jamii na wanasisitiza umuhimu wa muktadha wa matumizi ya lugha. Ni muhali usemi kuwa zao la mtu mmoja. Usemi huongozwa na tofauti za kimamlaka ambazo ni sehemu ya jamii. Tofauti hizi zimeshughulikiwa

katika utafiti huu kwa kurejelea jinsi lugha inavyowapa mamlaka waliokeketwa ilhali inawanyima mamlaka fulani wale ambao hawajatahiri. Hali hii imechunguzwa kwa misingi ya utambulisho wa kijamii ambao unapewa wasichana waliotahiri.

Nadharia hii hujihusisha na jinsi ambavyo wanajamii hupata na kuendeleza uwezo na mamlaka katika jamii husika, hubainisha utendakazi wa itikadi katika taasisi za kijamii na vile vile huonyesha jinsi ambavyo usemi huundwa na kuongoza mielekeo na mitazamo ya wanajamii. Hali hii imechunguzwa katika utafiti wetu kwa kuangazia usemi wa wanawake kuhusu ukeketaji na jinsi unavyoathiri uendelezaji wa mila hii. Aidha, matini zinazozungumzia ukeketaji wa wanawake zimefafanuliwa, hasa nyimbo za tohara, ili kuchunguza utendakazi wa asasi hii ya ukeketaji katika jamii ya Abagusii na jinsi utendakazi huu unavyoathiri mielekeo na mitazamo ya wanajamii hivi kwamba imekuwa kizungumkuti kuitupilia mbali mila hii licha ya madhara yake mengi kwa jamii.

Van Dijk (1986:4) anasema nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Wa Usemi huzingatia matatizo mbalimbali ya kijamii. Kwa kufanya hivyo huchanganua mtazamo wa wale ambao hutwezwa na kuchanganua mchango wa vipengele mbalimbali vya lugha vinavyotumika katika kuhalalisha mila hii katika matini za ukeketaji.

Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Wa Usemi imejengeka kwenye dhana nne muhimu: uwezo/mamlaka, historia, muktadha na itikadi. Hivyo basi kila usemi na matini katika lugha husika hubainisha historia na mielekeo ya jamii. Hii ni kwa sababu usemi na matini huwa na maana katika kipindi fulani cha kihistoria na katika muktadha mahususi. Usemi huhalalishwa na itikadi za jamii hasa na kundi la jamii lenye kumiliki mamlaka katika jamii.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti ametoa maelezo kuhusu mbinu zilizotumika katika ukusanyaji wa data na uteuzi wa sampuli. Utafiti huu ulikuwa wa nyanjani ambapo mtafiti aliendá uwanjani na kusikiliza nyimbo zilizoimbwa katika shughuli za ukeketaji ili kupata athari ya nyimbo hizo katika kukuza asasi ya ukeketaji. Mtafiti amegawa sura hii katika sehemu nne: Mahali pa Utafiti, Muundo wa Utafiti, Uteuzi wa Sampuli na Mbinu za Uchanganuzi wa data.

## 3.2 Muundo wa Utafiti

Data iliyokusanywa ilikuwa nyimbo za ukeketaji wa wanawake. Ukusanyaji wa data ulifanywa kwa kutumia muundo wa uchunguzi wa kimaelezo ambapo nyimbo zilizoimbwa katika shughuli za unyago zilinaswa kwa kutumia mwongozo wa mahojiano, kinasa sauti na kanda za kunasa sauti. Nyimbo hizi zilinaswa kutokana na vikao vitano vya makundi teule vilivyoteuliwa na mtafiti. Jambo hili lilimsaidia mtafiti kupata sifa mahsusi za lugha zilizojitokeza katika nyimbo za tohara. Aidha, ilimsaidia kupata maudhui yanayojitokeza katika nyimbo hizi. Kurekodi huku pia kulimwezesha mtafiti kupata msamiati unavyojitokeza na kuwasaili wahojiwa papo hapo ambapo hakuuelewa msamiati fulani vizuri.

## 3.3 Mahali pa Utafiti

Utafiti ulifanywa katika Wilaya ya Nyamira. Hii ni kwa sababu sampuli iliyopatikana hapa ni wakilishi kamilifu ya desturi hii kwa jamii ya Abagusii popote walipo.

## 3.4 Uteuzi wa Sampuli

Uteuzi uliofanywa hapa ulikuwa wa kimakusudi ili kukidhi madhumuni ya utafiti wetu. Mtafiti aliteua makundi matano ya wanawake, kila kikundi kikiwa na wanawake sita. Kila kundi liliteuliwa kuegemea tarafa tano zilizoko katika wilaya ya Nyamira. Wanawake hawa walikuwa kati ya umri wa miaka 35-80. Hii ni kwa sababu hawa walielewa vizuri mada ya utafiti, hivyo wangetoa habari za kina ambazo zingetosheleza mada hii. Kwa kuongozwa na mwongozo wa mahojiano aliyouunda, mtafiti aliwaongoza wahojiwa katika kupata nyimbo zilizoimbwa katika hatua mbalimbali za shughuli ya ukeketaji katika jamii husika. Hii ilituwezesha kuchanganua

maswala ya kihistoria, imani na mila yanayochangia ukeketaji wa wanawake katika jamii husika.

Akiongozwa na viongozi wa vijiji, mtafiti aliweza kuwapata wanawake hawa na kujieleza kwao ili wawe na uhuru wa kutoa habari zilizohitajika. Tarafa tano zilizoko katika wilaya Nyamira ziliteuliwa ili mtafiti aweze kupata sampuli ya nyimbo ya eneo lote la utafiti. Aidha, wilaya ya Nyamira iliteuliwa kwa vile imesheheni koo zote za jamii ya Abagusii. Kwa hivyo, tuliyokusanya yaliweza kuwakilisha na kuwasilisha imani, mielekeo na mitazamo ya jamii yote ya Abagusii hasa kuhusu ukeketaji.

Nyimbo kumi na sita zilikusanywa lakini mtafiti aliteua nyimbo kumi kimakusudi kama matini za kuchanganuliwa. Uteuzi huu ulimulikia uzito wa maudhui ambayo yangetuwezesha kuafikia madhumuni ya utafiti wetu.

### 3.5 Uchanganuzi wa Deta

Hatua ya kwanza iliyochukuliwa na mtafiti katika uchanganuzi wa deta ilikuwa ni kutafsiri deta iliyokusanywa kutoka kwa lugha ya Ekegusii hadi lugha ya Kiswahili. Hii ilitokana na ukweli kwamba, deta yote iliyonukuliwa ilikuwa ya lugha ya Ekegusii. Kisha, deta hii ilichanganuliwa kwa kuegemea madhumuni ya utafiti wetu na hatua tatu za uchanganuzi zilizopendekezwa na Norman Fairclough katika nadharia ya uchanganuzi hakiki wa usemi, yaani: Ufafanuzi, Ufasili na Upambanuzi.

Ufafanuzi wa sifa rasmi za matini teule ulifanywa kwa kuangazia matumizi ya takriri, jazanda, nomino na vivumishi. Isitoshe, ufafanuzi huu ulimulikia vile sifa rasmi zilivyoathiri mielekeo kuhusu ukeketaji hivyo kuchochea hamu kubwa kwa kila msichana kutamani kutahiriwa.

Aidha, ufasili wa utambulisho wa jamii katika ukeketaji ulifanywa kwa kuangazia mada tano zilizojitokeza katika matini mbalimbali za usemi huu. Mwingiliano kati ya matini na usemi uligusiwa pia.

Hatimaye, katika kuchanganua ujenzi wa mahusiano na utambulisho wa kijamii, mikakati ya lugha iliyodokezwa na Wodak na Meyer (2001:73) ilitumiwa. Mikakati hiyo mitatu ni:

a.) Unominoshaji

b.) Uvumishaji

c.) Kimjadala

Mikakati hii mitatu ilitumiwa ikiegemezwa kwa maudhui tano yaliyoteuliwa ili kudhihirisha ujenzi wa mahusiano na utambulisho wa kijamii katika matini kumi zilizoteuliwa.

Mkakati wa unominoshaji huangazia ujenzi wa uanachama katika makundi. Uanachama huu huundwa waziwazi au kwa kukisia. Tumeutumia mkakati huu kuchanganua jinsi ukeketaji unavyomsaidia aliyekeketwa kuingia katika kikundi cha wanaoheshimiwa na kutukuzwa katika jamii na vile anayepuuza mila hii anavyotengwa na kikundi hicho.

Mkakati wa uvumishaji huangazia uwasilishaji wa washiriki kichanya na kifinyu. Kwa kutumia mkakati huu tumechanganua jinsi aliyekeketwa anavyopewa sifa chanya katika jamii ya Abagusii na jinsi anayeipuuza mila hii anavyopewa sifa za kumtweza.

Mkakati wa kimjadala unashughulikia uhalalishaji wa sifa chanya anazopewa aliyekeketwa na sifa hasi anazopewa ambaye hajatahiri. Mbinu ya majadiliano imetumiwa kukuza uhalali wa sifa hizi.

# SURA YA NNE

# UCHANGANUZI WA DETA

## 4.1 Utangulizi

Katika sura hii tumechanganua deta kulingana na madhumuni ya utafiti. Mtafiti amechanganua sifa za lugha katika matini kama vile; takriri, jazanda, nomino na vivumishi. Aidha, amefasili utambulisho wa jamii katika usemi wa ukeketaji kwa kuegemea mada tano zilizotambuliwa na mtafiti. Hatimaye amepambanua athari za lugha katika ukeketaji.

## 4.2 Sifa za Lugha Katika Matini

Sifa nne za lugha zilizojitokeza zimefafanuliwa katika sehemu hii. Sifa hizo ni pamoja na: takriri, vivumishi, nomino na jazanda.

### 4.2.1 Matumizi ya Takriri

Takriri ni ule urudiaji wa silabi au sauti au maneno yanayolingana katika maneno yanayofuatana au yanayokaribiana kimatamshi. Takriri imetumika kusisitiza hoja au ujumbe, kudhihirisha hisia za waimbaji na kudumisha usuli wa wimbo. Mbinu hii imetumiwa kwa madhumuni hayo matatu katika takribani matini zote tulizomulikia katika utafiti wetu.

Katika matini ya kwanza, maneno *oyaye oyee (*naam imekuwa*)* yamerudiwa katika kila ubeti ili kusisitiza ujumbe unaomulikiwa katika kila ubeti wa matini hiyo. Kwa mfano, lahani katika ubeti wa tatu mshororo wa pili asemapo *orenge mokabaisia* waimbaji huitikia *oyaye oyee* kama ishara ya kukubaliana na ukweli kwamba mtahiriwa alikuwa mke wa watoto na sasa amekuwa mke wa wanaume. Ndiposa pia katika ubeti uo huo mshororo wa tatu lahani *asemapo obeire mokabamura* waimbaji wanaitikia *oyaye oyee*. Msisitizo huu unadhihirika katika wimbo wote na unatimiza majukumu mawili: kusisitiza ujumbe unaoimbiwa na kudhihirisha hisia za waimbaji kuhusu ukeketaji.

Katika matini ya nane, maneno hata sentensi yamerudiwarudiwa ili kusisitiza ujumbe wa wimbo husika. Kwa mfano, katika kiitikio cha wimbo huu umuhimu wa kutahiriwa na kujamiiana unasisitizwa:

*Oyotakama, oyaye oyotakama, oyaye*

*Oyotakama ebing'are biaye bioma*

Tafsiri:

Asiyekama, ndio asiyekama, ndio

Asiyekama watoto wake watakufa

Hapo waimbaji wamesisitiza kupitia mbinu ya takriri ya maneno asiyekama kuwa anayepuuza tohara watoto wake watakufa. Hivyo kuwatisha wasichana ambao wangefikiria kuasi tohara kuwa hawatapata baraka za watoto. Mifano zaidi ya matumizi ya takriri itapatikana katika viambatisho.

### 4.2.2 Matumizi ya Vivumishi

Vivumishi vya kawaida hutoa maelezo zaidi kuhusu nomino au viwakilishi kwa kuonyesha muundo, hali, tabia, kimo au idadi yao. Katika utafiti wetu, tumebainisha vivumishi ambavyo vimetumiwa katika matini mbalimbali kubainisha hali, tabia au kimo cha aliyetahiri ukilinganisha na yule ambaye hajatahiri.

Katika matini ya kwanza, kwa mfano, vivumishi vifuatavyo vimejitokeza: Katika ubeti wa 2, mshororo wa 3 kivumishi *Omosera* kimejitokeza kuelezea kuwa aliyetahiri amekuwa msichana muungwana baada ya tohara, sifa ambayo hakuwa nayo kabla ya tohara. Aidha, ubeti wa 4, mshororo wa 3, waimbaji wanasema:

*Abe mokungu muya*

Tafsiri:

Awe mke mwema

Hii inamaanisha kuwa baada ya msichana kutahiriwa anakuwa mke mwema, sifa na hali ambayo yule hajakeketwa hana.

Matini ya tano hali kadhalika imedokeza vivumishi vifuatavyo:

Rero n'ekegeni **kiao**

Tafsiri:

Leo ni sherehe **yako**

Hii ni katika ubeti 1, mshororo 3, ambapo wanamwimbia mzazi wa mtahiriwa kuwa siku hiyo sherehe ilikuwa yake. Kivumishi kimilikishi 'yako' kinamfanya mzazi huyo naye ajihisi kuwa ni wa muhimu zaidi kwa kuwafanya halaiki ya watu wa jamii yake kujumuika kwake ili

kushangilia tohara ya mwanawe. Kuimbiwa na kusifiwa huku kunampa motisha ya kuendelea kutahiri watoto wengine ili asifiwe tena. Aidha, wazazi wengine ambao hawajatahiri wasichana wao wangependa wawatahiri ili nao watunukiwe sifa hizi.

Isitoshe, katika ubeti1 mshororo wa 3, waimbaji wanasema:

*Nonya* ***mbike*** *igo toe*

Tafsiri:

Hata **vichache** tupe

Hapa kivumishi cha idadi 'vichache' kinamhimiza mzazi atoe chakula hata kidogo alicho nacho. Hii inamaanisha kuwa tohara iliambatanishwa na kutoa vyakula ambavyo vinaombwa katika wimbo huu. Katika utamaduni wa Abagusii, kutoa chakula kwa halaiki ilimpa mwanajamii sifa ya kutokuwa bahili na hivyo kuheshimiwa. Kwa hivyo kuhimizwa kutoa chakula hata kidogo ni ishara ya heshima uliyotunukiwa na wanajamii (waimbaji).

Katika matini ya nane, katika kiitikio chake waimbaji wanasema:

*Oyotakama, ebing'are* ***biaye*** *bioma*

Tafsiri:

Asiyekama watoto **wake** watakufa.

Hii inamaanisha kuwa ambaye hatatahiri na hasa kufuatana na mila na desturi za Abagusii basi watoto wake wangekufa. Ujumbe huu uliwaogofya ambao wangefikiria kuasi ukeketaji.

Matini ya tisa, ubeti wa 5 mshororo wa 2 waimbaji wanadai:

*Tiga ebuge yatiga abana* ***baye***

Tafsiri:

Wacha ilie imeacha watoto **wake**

Hapa inamaanisha kuwa aliyekuja ambaye ni mkubwa wa mtahiriwa, ananguruma kwani ameacha watoto wake, kumaanisha hata mtahiriwa angepata baraka za kupata watoto ikiwa angezingatia kanuni za tohara.

Isitoshe, matini ya kumi, ubeti wa mwisho, mshororo 2 na 3, vivumishi vifuatao vimejitokeza:

*Abana* ***bao*** *bakwe* - watoto **wako** wafe.

*Omogaka* ***oo*** *akwe* - Bwana**ko** afe.

Vivumishi vimilikishi hivi vinaashiria kuwa ikiwa mtahiriwa atatoboa siri za tohara kinyume na alivyoapa, basi watoto wake na hata bwanake wangekufa. Kiapo hiki kinafanya wasichana wengi hasa wale ambao hawajatahiri kuwa na hamu kubwa ya kupitia tohara hili nao wapewe siri hizo, kwani hawangezipata kwa waliotahiri.

### 4.2.3 Matumizi ya Nomino

Nomino hutaja kitu, mtu, hali, kiumbe, cheo, dhana, mahali na tendo. Hufanya kazi ya kutambulisha kitu kinachotajwa, kukibainisha na kukitofautisha na vitu vingine. Katika utafiti wetu, tumebainisha nomino mbalimbali ambazo zinawatambulisha na kuwatofautisha waliotahiri na ambao hawajatahiri.

Kwa mfano, katika matini ya kwanza, nomino zifuatazo zimetumiwa kumsifia aliyetahiri: katika ubeti 3, mshororo 3, wanadai:

*Obeire* ***omoiseke*** *omosera*

Tafsiri:

Awe **msichana** muungwana

Kinyume na ambaye hajatahiri, ambaye hudunishwa na kuitwa kisichana, aliyetahiri anasifiwa na kuitwa msichana muungwana. Katika ubeti 3, mshororo 3, wanadai:

*Obeire* ***mokabamura***

Tafsiri:

Amekuwa **mke wa vijana** chipukizi

Hapa wanamsifia aliyetahiri kuwa amekuwa mke wa vijana chipukizi wala si mke wa watoto, alivyokuwa kabla ya kutahiriwa. Hii hadhi mpya kila msichana anaipapia hivyo ahitaji tohara ili kuipata.

Aidha, ubeti 4, mshororo 3 , wanamsifia aliyetahiri kwa kusema:

*Abe* ***mokungu*** *muya*

Tafsiri:

Awe **mke** mzuri

Hapo amepewa jina 'mke' ambayo ni hadhi mpya atakuwa nayo kwa vile ametahiriwa. Na hivyo majukumu yanayoambatana na hadhi hiyo mpya atatwikwa.

Ndiposa katika ubeti wa 5 mshororo 2 na 3 waimbaji wanasema:

***Abamura*** *bamoire* – **Wavulana chipukizi** wamchukue

*Anyore* ***abana*** – Apate **watoto**.

*Arosie* ***egesaku*** – Aendeleze **kizazi**.

Katika vifungu hivyo, aliyetahiri amepewa majukumu yafuatayo: Kwanza, aweze kuolewa na wavulana chipukizi si wazee au watoto. Pili, akishaolewa amepewa jukumu la kupata watoto na kuendeleza kizazi cha jamii ya Abagusii. Haya yote yanamtambulisha aliyetahiri kama mwanajamii ambaye amepata hadhi ya juu na majukumu makubwa kinyume na asiyetahiri. Hivyo basi, kuwapa motisha wale ambao hawajatahiri kungojea siku ya kutahiri ili nao wapandishwe hadhi.

Isitoshe, katika ubeti 6 mshororo 3 waimbaji wanasema aliyetahiri:

*Otigire* ***egosorio*** – Ameacha **mzaha**

Hii nomino *egosorio* inadhamiria kuonyesha kuwa mtahiriwa amekuwa mtu mkubwa ambaye haruhusiwi kushiriki mizaha ya kitoto kwani yeye si mtoto tena. Hivyo nomino hiyo inaashiria hadhi mpya ya utu uzima aliyoipata mtahiriwa.

Katika matini 3 nomino zifuatazo zimetumiwa kumsifia aliyetahiriwa; Ubeti 4 mshororo 1 wanasema:

*Obeire* **omoiseke** – Amekuwa **msichana**

Hapa wasisitiza ukweli kuwa aliyetahiri amekuwa msichana si mtoto tena. Hivyo ametwikwa hadhi mpya yenye taadhima kuu. Ndiposa katika ubeti 5 mshororo 1 wanasema kuwa aliyetahiri amemiliki heshima ambayo asiyetahiri hamiliki:

*Atware* ***amaskani*** – Awe na **heshima.**

Aidha, katika matini 5 ubeti 4 mshororo 1 waimbaji wanasema:

*Ekio* ***omogoko*** *toe* – Cha **bahili** tupe

Nomino 'bahili' imetumika kuakisi yule ambaye hatahiri watoto wake kwa sababu sherehe za tohara zilihusishwa na utoaji wa vyakula kwa wanaohudhuria. Hivi kwamba ambaye hataki kutahiri ni ishara ya kuwa mchoyo, yaani hataki kutoa vyakula kwa wanajamii. Hii ni sifa kila mmoja angetaka kujiepusha nayo kwa kushiriki katika shughuli ya kutahiri watoto wake. Nomino hii pia inajitokeza katika matini 6 ubeti 3 mshororo 1.

Katika matini 7 ubeti 1 mshororo 3; ubeti 2 mshororo 2 na ubeti 3 mshororo 2; msichana aliyetahiri anaitwa '***makomoke***' - ' shangazi'. Nomino 'shangazi' inaashiria heshima kubwa kwake. Kwingineko katika matini ii hii nomino hii imehusishwa na jukumu la kuwa mkulima ambaye anawalisha wote hata wapita njia.

Katika matini 8 ubeti 2 mshororo 1, wanasema:

*Ngochia bw'omogaka nganye **ebisi***

Tafsiri:

Nikiolewa kwa mzee nikamue kwa **zamu**.

Hii nomino '***ebisi***' inamaanisha kuwa ambaye hajatahiri ataolewa na mzee na hivyo atakosa uhondo kamili wa ndoa ikilinganishwa na aliyetahiri ambaye ataolewa na kijana chipukizi. Hivyo kila msichana aling'ang'ania kutahiriwa ili aozwe kwa kijana chipukizi. Kwingineko katika ubeti 3, mshororo 1 hali hii inasisitizwa ambapo aliyetahiri hatarajiwi kuolewa na mzee kwani atakuwa kama 'kipofu' yaani yule ambaye hajatahiri. Kwa hivyo msichana alitazamia kutahiriwa ili asiozwe mzee kana kwamba yeye ni kipofu. Hivyo ambaye ametahiriwa hufunzwa kumchagua mume mwenye sifa nzuri na aliye chipukizi wala si mwenye sifa mbaya au mzee asiye na uwezo wa kukimu mahitaji yake ya kimwili na kimaisha kwa jumla. Ndiposa anahimizwa katika ubeti 2, mshororo 2 na ubeti 3, mshororo 2 kuwa:

*Ngochia bw'omomura nkame **nyamasi***

Tafsiri:

Nikiolewa kwa mvulana nikamue **ng'ombe mnono**

Hapa inamaanisha aliyetahiri hufanya uchaguzi mwema wa mchumba kwani amefunzwa akiwa jandoni. Haya yamedhihirika katika wimbo huu wa sherehe ya mahafali.

Katika matini 9, ubeti 1, mshororo 2 , na ubeti 2 , mshororo 1 wanasema kuwa:

*Nyamaruma n'eng'ombe ekoa **mwana***

Tafsiri:

Akinguruma ni ng'ombe anayemlisha **mtoto**

Nomino 'mtoto' imetumiwa kuashiria kuwa anayetahiri hupata baraka ya kupata mtoto kinyume na ambaye hajatahiri. Hali kadhalika nomino kama vile '*egesagane*' imetumika kumdunisha ambaye hajatahiri. Kwa mfano, matini 1, ubeti 2, mshororo 2, waimbaji wanasema:

*Orenge* ***egesagane*** – Alikuwa **kisichana**

Hii inamaanisha kuwa ambaye hajatahiri ni kisichana na hivyo hadhi yake ni ya chini na angevuka daraja hadi hadhi ya juu ikiwa angetahiriwa.

Aidha, katika matini 1, ubeti 3, mshororo 2, wanasema:

*Orenge* ***mokabaisia*** – Alikuwa **mke wa watoto**

Hapa inamaanisha kuwa akiwa bado kutahiriwa alikuwa anashiriki mizaha na watoto ndiposa wakamwita mke wa watoto. Lakini sasa ikiwa ametahiri hawezi kushiriki tena mizaha na watoto bali ataolewa na wanaume chipukizi ambao watamfaa katika kuendeleza kizazi cha jamii.

### 4.2.4 Matumizi ya Jazanda

Jazanda ni tamathali ya usemi ambayo inatumia maneno (sana sana kistiari) kujenga picha zinazoibua hisia katika ushairi simulizi (nyimbo). Katika utafiti wetu jazanda mbalimbali zimetumiwa katika kuibua hisi za mtahiriwa kuwa yeye ni bora kuliko wale ambao hawajatahiri.

Katika matini 2, kinembe kinarejelewa kuwa *egoto* (ubeti 2, mshororo 1) na *ekoko* ( ubeti 7, mshororo 1) kumaanisha uchafu. Maneno hayo yametumiwa kijazanda kuashiria kuwa kinembe ni 'kichafu' kwa sababu kikiguswa kinaweza kusababisha madhara kama vile aibu kwa kuvunja ubikira ikiwa msichana angeshiriki mapenzi kabla ya ndoa au kupata mtoto kabla ya ndoa na hivyo sifa nzuri za msichana zingeharibika.

Katika matini yiyo hiyo, aliyetahiri anapewa ruhusa ya kushiriki mapenzi. Ndiposa anasifiwa kuwa yeye amegusa kinembe katika wakati wake.Kwa hivyo, ana fursa ya kushiriki mapenzi ndani ya ndoa baada ya kufuzu. Ndiposa anaimbiwa:

*Gwakunire bionsi, kuna* – Umegusa vyote, gusa

Hapa 'vyote' inamaanisha kuwa baada ya kutahiri mtahiriwa ana uhuru wa kuolewa na kushiriki mapenzi ndani ya ndoa. Kwingineko katika matini yiyo hiyo kinembe kinaitwa '*enyambu*' (ubeti 4, mshororo 1) yaani lumbwi. Hii inamulikia 'utakatifu' wa sehemu za uzazi za wasichana kulingana na jamii ya Abagusii. Waliamini kugusa kinembe kunaleta ashiki za mapenzi. Jazanda ya kinyonga inadhamiria kuonyesha hisia mbalimbali ambazo huibuliwa kutokana na mguso wa kinembe.

Katika matini 8, neno '*enchage*' limetumiwa kijazanda kumaanisha dhakari. Wimbo huu unasema kuwa aliyetahiri ana uhuru wa kujamiiana na mwanamume ili apate watoto. Asipofanya hivyo hapati watoto. Ndiposa wanaimba:

*Kama enchage k'eng'ombe ekoe mwana*

Tafsiri:

Kama ng'ombe akupe mtoto

Naye msichana aliyetahiri anafananishwa kijazanda na ng'ombe, kuwa akishiriki mapenzi na mwanamume bila shaka atapata mtoto. Asiposhiriki mapenzi au asipoolewa baada ya tohara hawezi kupata watoto. Ndiposa wanaimba:

*Oyotakama ebingare biaye bioma*

Tafsiri:

Asiyekamua watoto wake watakauka

Hii inamaanisha kuwa akishiriki mapenzi kabla ya tohara watoto wake watakufa. Pia inaashiria kuwa asiposhiriki mapenzi katika ndoa basi hatabahatika kupata watoto. Hii ni kwa sababu msichana pekee hawezi kupata mtoto bila mbegu za mwanaume. Ruhusa ya kushiriki mapenzi anaipata baada ya tohara.

Jazanda nyingine imejitokeza katika matini 9, ambapo jina *'nyamaruma'* limetumika kuashiria msichana ambaye ametahiri na yuko karibu kufuzu. Anaambiwa sasa ana uhuru wa kufurahia mapenzi katika ndoa kwani ametayarishwa kwa muda mrefu na ametosha. Anashauriwa kuwa akifurahia mapenzi ndani ya ndoa basi atapata watoto.

Katika matini 4, msichana aliyetahiri anafananishwa kijazanda na nyota (*mongesa*). Hii ni kwa sababu sasa amefuzu na hivyo yeye ni 'nyota' ya jamii ambayo kwayo wengine wangeona faida ya tohara na kizazi cha jamii kitaendelezwa. 'Nyota' hii itaongeza joto katika jamii kwa njia hii kupoteza baridi *(bokingite)*, kuonyesha mchango wa aliyetahiri katika kuendeleza kizazi.

## 4.3 Ufasili wa Utambulisho wa Jamii katika Ukeketaji

Katika hatua hii tumeangazia uhusiano kati ya matini na maingiliano (tendo la usemi). Uhusiano huu umefasiliwa kwa kuangazia mada zinazojitokeza katika matini mbalimbali za usemi huu na jinsi mada hizo zimejenga utambulisho na mahusiano katika jamii. Mikakati mitatu kati ya mitano iliyodokezwa na Wodak na Meyer (2001) imetumiwa kutathmini ujenzi wa utambulisho huu. Mikakati hiyo ni: Unominoshji, Uvumishaji na Kimjadala.

### 4.3.1 Mada za Usemi wa Ukeketaji

Usemi wa ukeketaji ulidokeza mada mbalimbali. Uteuzi wa mada ulikuwa muhimu katika kuakisi uwezo. Yaani, uwezo wa kuamua maingiliano ya usemi huhusu nini. Msikilizaji hana la kutia katika mada hiyo inayozungumzia usemi huo. Jamii ina madhumuni yake ya

kurithisha mila na desturi zake ambazo wangetaka wasikilizaji wazipate, ndiposa usemi wa ukeketaji una mada teule. Kwa hivyo, waimbaji na wasikilizaji hushiriki tendo la usemi na muktadha wa usemi ambao una mada ambazo hawana uwezo wa kuzidhibiti. Tangu mwanzoni, fikira zimeelekezwa mkondo mmoja. Mshiriki hapewi fursa ya kushiriki nje ya mipaka. Mada hizo ni pamoja na:

i) Uke na ndoa
ii) Uvumilivu
iii) Heshima na Hadhi
iv) Utamaduni
v) Ukarimu

Nyimbo zote kumi ambazo zimetathminiwa, zimefanywa hivyo kwa misingi ya mojawapo au muungano wa mada hizi.

### 4.3.2 Mwingiliano Kati ya Matini na Usemi

Mwingiliano na mahusiano kati ya matini na mada za usemi wa ukeketaji husheheni sehemu ya muktadha wa usemi huu. Matini kwa njia ya moja kwa moja au vinginevyo huweza kurejeleana. Vilevile, matini zaweza kuwa na mihimili ya mada zinazolingana. Mahusiano hayo yanaweza kuonyeshwa katika jedwali lifuatalo. Katika jedwali hili matini zimerejelewa kwa kutumia nambari zilizopewa katika maelezo, yaani, nambari 1-10.

**Jedwali 3: Maingiliano Kati ya Matini na Usemi**

| MADA YA MDAHALO | MATINI |
|---|---|
| Uke na Ndoa | 1,2,3,8 |
| Uvumilivu | 8,9 |
| Heshima na Hadhi | 1,2,3,4,6,7,8 |
| Kutukuza utamaduni | 1,2,7,8,10 |
| Ukarimu | 3,5,6 |

Asili: Deta ya Nyanjani 2007

## 4.4 Matumizi ya Mikakati ya Lugha Katika Ujenzi wa Utambulisho wa Kijamii

Mtafiti alianza kwa kuhakiki lugha katika matumizi. Hii ilijumuisha utambulisho wa nyanja ambazo kwazo utambulisho ulijengwa. Mikakati mbalimbali ya lugha iliyotumiwa kujenga utambulisho wa jamii ulitambulishwa. Uchanganuzi ulihusisha matumizi ya mikakati ya lugha ilivyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 4: Mikakati ya Lugha katika Ujenzi wa Utambulisho**

| Mikakati ya Lugha | Madhumuni | Mbinu za Lugha |
|---|---|---|
| **Unominoshaji** | Ujenzi wa uanachama katika makundi | • Makisio |
| **Uvumishaji** | Uwasilishaji wa washiriki kichanya na kifinyu | • Jazanda/Sitiari<br>• Makisio<br>• Uteuzi wa msamiati |
| **Kimjadala** | Uhalalishaji wa sifa chanya na finyu | • Matumizi ya ukweli wa mambo na majadiliano |

Asili: Wodak, R na M. Meyer (eds) (2001:73)

### 4.4.1 Uke na Ndoa

Tulijadili mikakati ya lugha iliyotumika kuunda utambulisho wa jamii kuhusu uke na ndoa. Mikakati hiyo ni pamoja na : Unominoshaji, Uvumishaji na Kimjadala.

#### 4.4.1.1 Unominoshaji

Usemi wa ukeketaji huunda uanachama katika kikundi waziwazi au kwa kukisia. Matini 1 imemtambulisha aliyetahiri ikitumia nomino mbalimbali za kuashiria uke na ndoa. Kwa mfano;

*Obeire* ***omoiseke*** *omosera*

Tafsiri

Amekuwa **msichana** mzuri

Inamaanisha kuwa kabla ya tohara msichana hakuhesabiwa kuwa msichana mzuri. Ujumbe huu unammotisha msichana ambaye hajatahiri naye awe katika kikundi cha wasichana wazuri. Na kwa njia hiyo aweze kupewa majukumu yanayoambatana na uke na ndoa. Hivyo, kila msichana hungojea kwa hamu hiyo siku ya kutahiri naye atambuliwe kuwa msichana mzuri.

Kwingineko katika matini ii hii msichana aliyetahiri alitiwa katika kundi la wake wazuri. Waimbaji wanasema:

*Abe* ***mokungu*** *muya*

Tafsiri:

Awe **mke** mzuri

Kifungu hiki kinamtambulisha aliyetahiri na mke mzuri katika jamii. Hii inamaanisha kuna kikundi kingine cha wake wabaya. Hivyo waimbaji wanadhamiria kumtambulisha aliyetahiri na kikundi cha wake wazuri. Aliyeasi desturi hii ya tohara alitambulishwa na kikundi cha wake wabaya wanaoiasi mila za Abagusii. Hii inammotisha msichana ang'ang'anie tohara ili naye ajitambulishe na kikundi cha wake wazuri.

Isitoshe, katika matini yiyo hiyo, waimbaji wanadai:

*Obeire* ***mokabamura***

Tafsiri

Amekuwa **mke wa wavulana**

Kifungu hiki kinadai kuwa aliyepitia tohara amekuwa mke wa wavulana chipukizi. Wavulana ni vijana. Ujana uliakisiwa kuwa mzuri. Anayeolewa na vijana huwa amepata mume mzuri ilhali aliyeolewa na wazee na kushiriki mapenzi na ambaye hajatahiri alihesabiwa kuwa kikundi duni. Na kikundi hiki ni cha wale ambao hawajatahiri au ikiwa wametahiri huwa walivunja kanuni fulani za desturi hii kama vile aliyelia *(enkuri)* alilaaniwa kuwa aolewe na wazee. Hivyo kila mmoja alikazania tohara ili ajitambulishe na wengine ambao wangeolewa na vijana chipukizi.

Katika matini 2, aliyetahiri anaambiwa 'amegusa vyote' kumaanisha anaweza kuolewa na kushiriki mapenzi. Hii inaashiria kuna kikundi ambacho hakiruhusiwi kugusa vyote yaani kushiriki uke na ndoa. Kila msichana angependelea kujitambulisha na kikundi kunachoruhusiwa kushiriki uke na ndoa (kugusa vyote), hivyo kukazania tohara.

Katika matini 6 aliyetahiri anatambulishwa kama:

'Mama aliyebarikiwa na anaweza kuona kifungua mimba'

Hii inamaanisha kuna mama ambao hawajabarikiwa, hivyo hawapati watoto. Waimbaji wanamtambulisha aliyetahiri kuwa kikundi cha wale mama waliobarikiwa na ambao wanaweza kupata watoto kinyume na asiyetahiri. Jambo hili lilikuwa msukumo wa wasichana kukazania tohara ili nao wajiunge na kikundi hiki kilicho na baraka.

Katika matini 8 waimbaji wanasema:

'Kama ng'ombe akupe mtoto'

Usemi huo unampa ruhusa 'akame' ndipo apate mtoto. Hii inaashiria kuna kikundi cha wale ambao hawaruhusiwi kukama ndiposa wapate watoto. Hapa aliyetahiri anatambulishwa kuwa katika kikundi kinachoweza kukama na kupata watoto. 'Kukama' kunamaanisha kuwa ana uhuru wa kushiriki mapenzi ndani ya ndoa ili apate watoto kinyume na asiyetahiri. Hivyo, kila msichana angeng'ang'ania kutahiri ili aweze kujitambulisha na kikundi cha wale ambao wanaweza kushiriki mapenzi ndani ya ndoa ili wapate watoto.

#### 4.4.1.2 Uvumishaji

Utambulisho wa kijamii na kikundi fulani uliolezewa, umeakisiwa kichanya na kifinyu. Katika matini 1, waimbaji wanadai aliyetahiri:

'Alikuwa kisichana, amekuwa msichana' (Ubeti2, mshororo 2 na 3)

Kuwa kisichana ni dhana hasi ilhali kuwa msichana ni dhana chanya. Hii imejikita katika imani kuwa aliyetahiri ndiye msichana kamili ambaye angeshiriki majukumu ya uke na ndoa. Hali kadhalika asiyetahiri aliitwa kisichana kwa kuwa hawezi kushiriki uke wala ndoa.

Katika matini ii hii, waimbaji wanasema:

'Alikuwa mke wa vivulana, amekuwa mke wa wavulana'

Kuwa 'mke wa vivulana' ni dhana hasi ilhali 'mke wa wavulana' ni dhana chanya. Hii inaegemea katika ile imani kuwa aliyetahiri ndiye alikuwa na ruhusa ya kushiriki katika majukumu ya uke na ndoa, vinginevyo hashiriki majukumu hayo. Huu ujumbe wa waimbaji unawamotisha wasichana wengine kutamani kutahiriwa ili wapate sifa chanya ya kushiriki uke na ndoa.

Kwingineko katika matini ii hii wanasema:

'Apate watoto' (ubeti 5, mshororo 3)

Hapa aliyetahiriwa amepewa sifa chanya ya kupata watoto, kuashiria kuwa ambaye hajatahiri hana ruhusa kupata watoto. Dhana hii imejikita katika imani kuwa aliyetahiri ndiye mtu mzima

aliye na uhuru wa kushiriki ndoa na kupata baraka za watoto. Hili likiwa mojawapo la majukumu ya uke na ndoa na hasa baada ya kutahiri. Hii inadhihirisha kuwa aliyetahiri amepewa uwezo mkubwa kuliko ambaye hajatahiri. Hivyo, hili liliwafanya wasichana wengine wang'ang'anie tohara ili wapate uwezo huu.

Katika matini 2, aliyetahiri anaambiwa:

'Amegusa kinyonga' (ubeti 4, mshororo 1 )

Jazanda 'kinyonga' inaonyesha aliyetahiri ana uhuru wa kushiriki mapenzi katika ndoa. Kinembe kinafananishwa na kinyonga kwani kikiguswa hasa na dhakari ya mwanamume kinaweza kubadilisha hali ya ubikira ya msichana hata akapata mtoto. Pia kikiguswa na ngariba kinabadilisha hadhi kutoka utoto hadi utu uzima. Hivyo, aweza kushiriki mapenzi katika ndoa kinyume na ambaye hajatahiri. Hii inakuwa motisha kwa wasichana kutamani kupata uwezo huu, hivyo kutamani tohara.

Katika matini 3, waimbaji wanasema:

'Amekuwa msichana awezaye kuolewa'

Hii inaonyesha kuwa ambaye hajatahiri hana uwezo wala ruhusa kuolewa. Hivyo sifa ya kuolewa imetwikwa aliyetahiri. Kifungu hiki kinaashiria kuwa kila msichana anayehitaji kupata uwezo na ruhusa kushiriki ndoa sharti atahiriwe. Mng'ang'anio wa uwezo huu ndio hasa unakuza ukeketaji.

Katika matini 8, waimbaji wanasema:

'Anayekama ng'ombe ampe mwana
Asiyekamua watoto wake watakauka'

Hii inatoa sifa chanya kwa anayetahiriwa; kuwa aweza kupata watoto na waishi siku nyingi ilhali asiyetahiri hatapata watoto. Ndiposa wanasema asiyekama watoto wake watakufa. 'Kukauka' kunamaanisha asiyetahiri haruhusiwi kupata watoto au ikiwa amepata si halali hivyo wanaweza kufa. Hivyo kila msichana ilimbidi ang'ang'anie kupata watoto ndani ya ndoa ili naye ajitambulishe na sifa chanya. Hali hii basi iliendeleza ukeketaji.

#### 4.4.1.3 Mikakati ya Kimjadala

Hii ni mikakati ya kuhalalisha sifa chanya na hasi za waliotahiri na wasiotahiri. Katika mada ya uke na ndoa, majadiliano kadhaa yanadhihirika kuhalalisha sifa za kujitambulisha kijamii.

Katika matini 1, baada ya kumpa sifa chanya aliyetahiri, kuwa: amekuwa msichana mzuri, amekuwa mke wa wavulana, amekuwa mke mzuri na apate watoto; waimbaji wanatoa maoni yafuatayo:

'Ameacha mizaha'

Hii inamaanisha kuwa akishakuwa na sifa zilizotajwa hivyo hawezi kushiriki mizaha. Mizaha ilichukuliwa kuwa ya watoto wadogo. Hivyo basi ikiwa ameacha kushiriki mizaha ya kitoto, aweza kuwajibika katika majukumu ya uke na ndoa.

Kwingineko, katika matini 1 wanamsifu aliyetahiri kuwa:

'Mtoto amefanya vizuri'

Hii inaashiria kutahiri ni kufanya jambo chema. Hii inaonyesha kuwa ikiwa aliyetahiri amefanya vizuri anaweza kushiriki uke na ndoa.

Matini 8, waimbaji wanasema kuwa:

'Aolewaye na mzee akamue baadaye
Aolewaye na kijana akamue maziwa mengi'

Hapa waimbaji wanatoa mjadala unaohalalisha sifa chanya kuwa ikiwa unataka kukamua 'maziwa' mengi sharti utahiri ili uolewe na kijana. 'Maziwa' ni jazanda ya baraka kwa jamii ya Abagusii. Hivyo basi wasemapo kuwa anayetahiri ataolewa na kijana na akamue maziwa mengi wanamaanisha atapata watoto wengi na kupata baraka nyingi kinyume na asiyetahiri. Ambaye atakamua baada ya wengine kukamua, kumaanisha hatapata baraka nyingi kama wenzake katika kundi lile lingine. Hivyo, kila mmoja alikuwa na hamu kubwa ya kutahiriwa ili aolewe na kijana na kupata baraka nyingi.

#### 4.4.2 Uvumilivu

Tuliangazia pia mikakati mbalimbali ya lugha iliyotumiwa kuleta dhana ya uvumilivu.

##### 4.4.2.1 Unominoshaji

Waimbaji wa nyimbo za nyiso waliakisi vikundi tofauti ambapo kuna lile la waliotahiri ambao wanahesabiwa kuwa na uvumilivu na lingine la wale hawajatahiri ambao hawana sifa hiyo. Kwa mfano, matini 8, inasema:

'Asiyekamua watoto wake watakauka
Anayekamua ng'ombe wake akupe mwana'

Wanaashiria kuwa anayekamua ana sifa ya uvumilivu wa uchungu upatikanao katika tohara. Matokeo ya uvumilivu huo ni kupata watoto kinyume na ambaye hajatahiri. Yeye amekosa uvumilivu hivyo watoto wake watakauka (watakufa) au hatapata watoto.

Hivyo washiriki katika usemi huu wanahusisha uvumilivu na tohara, hivi kwamba tohara hukuza uvumilivu na uvumilivu huu huzaa matunda ambayo ni kupata watoto. Hii ni kuashiria kuwa bila tohara hupati watoto. Dokezo hili linawafanya wasichana wengi kuthamini tohara ili nao wapate baraka hii ya kupata uvumilivu ambao utavyaza tunu ya kupata watoto.

Katika matini 9, washiriki katika usemi huu wa ukeketaji wanasema:

'Wacha alie akilia malaloni'

Hapa mtahiriwa anaambiwa kuwa akilia fisi atamla. Ndio maana wanamtisha kuwa akilia pale jandoni, fisi ambaye anaendelea kunguruma atamla bila shaka. Hivyo kumaanisha kuwa asiye na uvumilivu na mwoga hashiriki tohara, akishiriki atapoteza maisha yake.

#### 4.4.2.2 Mikakati ya Uvumishaji

Sifa chanya na hasi pia zimetwikwa washiriki katika tohara hasa kuhusiana na dhana ya uvumilivu. Kwa mfano, waimbaji katika matini 8, wanasema:

'Kemunto kamua ndio Kemunto kamua'

Hapa Kemunto ni yule ambaye amekwishatahiri na ameonyesha uvumilivu. Kwa hivyo; ameruhusiwa kushiriki katika miviga ya tohara na pia kuwafunza watahiriwa wengine.

Vinginevyo, katika matini ii hii katika kiitikio wanaimba:

'Asiyekamua watoto wake watakauka'

Huyu ambaye hakamui anapewa sifa hasi ya kuwa watoto wake watakauka. Kumaanisha hawezi kuvumilia uchungu wakati wa kuzaa ikiwa hakuvumilia uchungu wa tohara na hivyo watoto wake huenda wakafa au asiweze kupata watoto. Haya yanaashiria kuwa baraka za kupata watoto ni za wale walitahiri wakifuata mila na desturi zilizokubalika katika jamii.

Isitoshe, katika matini yiyo hiyo, fisi anaambiwa achukue watu wa familia ya mtahiriwa lakini anakataa. Anasema atamchukua mtahiriwa hasa akilia.Ndiposa wanaimba:

'Mchukue mamake- la, Mchukue babake – la,

Mchukue mtahiriwa--- ndiooo

Maneno haya yanadhamiria kuwa fisi huyu angemchukua mtahiri ambaye ni mwoga- asiye na uvumilivu. Lakini ikiwa yeye si mwoga hangechukuliwa. Ndiposa fisi anakataa kuchukua

familia ya *omware* hasa hawa wakubwa kwa vile wao walikuwa wavumilivu katika tohara na hivyo wamefuzu na kupata hata watoto-yeye mtahiriwa akiwemo. Hapa pia mvumilivu ambaye ameshiriki na kufuzu tohara anamulikwa kama ambaye hatapoteza maisha yake, lakini asiye na uvumilivu hasa katika tohara ataliwa na fisi (atapoteza maisha yake).

Katika matini 5, wanaimba:

'Wacha angurume ameacha watoto wake'

Kifungu hiki kinaashiria kuwa fisi amewaacha watoto wake wakiwa njaa. Hivyo, endapo mtahiriwa angelia basi angekuwa kitoweo cha watoto wa fisi. Kifungu hiki kimeakisi anayeshiriki tohara kuwa jasiri na shupavu. Hii ni kwa sababu akiwa mwoga basi atapoteza maisha yake kwani atakuwa kitoweo cha fisi. Hapa yaelekea kuwa anayekataa kushiriki tohara ni mwoga. Hata wazazi wa yule ambaye hashiriki tohara wangechukuliwa kuwa woga. Hivyo, ili yeyote asipate sifa hii mbaya ya woga, wasichana wote na hata wazazi wote waliamini kushiriki tohara ili wasidharauliwe katika jamii.

#### 4.4.2.3 Mikakati ya Kimjadala

Katika kuhalalisha sifa hasi na chanya washiriki katika usemi wa ukeketaji wanatoa maoni kadhaa kimjadala katika dhana hii ya uvumilivu. Katika matini 8, wanasema:

'Kamua ng'ombe ee, kamua ng'ombe
Kamua ng'ombe ana maziwa mengi'

Tumejadili kuwa aliyeruhusiwa 'kukamua ng'ombe' ni yule asiye na woga, amevumilia maumivu ya tohara- kwa kifupi ameshiriki na kufuzu miviga yote ya tohara. Hili kuwatia moyo wengi washiriki tohara wanadai kuwa anayeshiriki tohara atapata watoto na atapata maziwa mengi. 'Maziwa' na 'watoto' ni ishara ya baraka katika jamii ya Abagusii. Ndiposa hata wakati *omware* alikuwa anafuzu baba alimtemea maziwa na kumwambia kuwa apate watoto wengi. Baraka kutoka kwa mababu kwa watoto katika jamii zilipitia kwa mzazi wa mtoto husika. Fursa ya kuzipata baraka imo katika tohara. Hivi kwamba asiye mvumilivu au aliye mwoga ambaye hajajishajiisha kushiriki tohara angekosa baraka hizi. Mahitaji ya baraka yanamsukuma kila mmoja akazanie tohara ambapo atapewa rasmi baraka hizi.

### 4.4.3 Heshima

Mikakati mitatu ya utambulisho wa kijamii yaani; unominoshaji, usifa na kimjadala imetumika katika kujenga utambulisho wa kijamii hasa kuhusu mada ya heshima.

#### 4.4.3.1 Mikakati ya Unominoshaji

Usemi wa ukeketaji huunda uanachama katika kikundi waziwazi au kwa kukisia. Katika matini 2, washiriki katika usemi wa ukeketaji wanamtambulisha aliyetahiri kama mtu aliyekamilika kwani 'amegusa vyote' vinavyostahili. Wanasema:

Umegusa vyote, gusa x 2

Gusa mwenzangu, mama gusa.

Hapa aliyetahiri anatambulishwa na wengine ambao wametahiri. Ndiposa wamemwita 'mwenzao' na pia 'mama'. Wanamwita 'mama' kwa vile ametahiri na astahili kuheshimiwa. Hivyo inaelekea kuwa ambaye hajatahiri hataimbiwa wimbo huu na hivyo hastahili heshima kama yule aliyetahiri. Majukumu mengine yanayoambatana na heshima hiyo atayatwikwa kinyume na ambaye hajatahiri.

Katika matini 3, ubeti wa 5 , mshororo 1, washiriki wanamtambulisha aliyetahiri kuwa atakuwa na heshima. Wanasema:

'Ee mwenzetu, awe na heshima

Kwa wote, ee mwenzetu' x 2

Vinginevyo ambaye hajatahiri anachukuliwa hana heshima (kwa watu wote) kwa vile hatakuwa amepitia mafunzo ambayo huambatana na tohara kulingana na mila na desturi. Hivyo aliyetahiri anapata utambulisho wa kijamii kama aliye na heshima na asiyetahiri kama mtu asiye na heshima.

Katika matini 4 aliyetahiri amepewa majina yanayoakisi heshima zake. Anaitwa 'mwanamke' na 'msichana'. Wanaimba:

'Mwanamke shangilia, naam

Tumekuletea msichana shangilia'

Majina haya yaliwapa utambulisho wa kijamii kama waheshimiwa ambao wanaweza kushiriki majukumu kadhaa ya jamii kama vile kuolewa, kulima, miongoni mwa majukumu mengine.

Heshima ni kitu kila mwanadamu hukitamani, hivyo, ile hali ya kutaka kujitambulisha na wanaotunukiwa heshima katika jamii wanakazania kuwachukua wasichana wao wakeketwe.

Katika matini 6, ubeti1, mshororo 1; washiriki katika usemi wa ukeketaji wanaimba:

'Mtenge mama aliyebarikiwa'

Hapa wanamtambulisha kijamii aliyetahiri kama 'mama aliyebarikiwa'. Huu utambulisho anampa heshima aliyetahiri. Heshima hiyo imeambatana na baraka. Ndiposa akaitwa mama aliyebarikiwa. Heshima na baraka zilitwikwa aliyetahiri. Katika harakati za kung'ang'ania heshima hii, kila msichana hutamani kukeketwa.

#### 4.4.3.2 Mikakati ya Uvumishaji

Kuhusiana na heshima aliyetahiri amepewa sifa chanya ilhali asiyetahiri amepewa sifa hasi- hasa kuhusiana na tunu ya heshima. Kwa kutumia jazanda ya 'kinyonga' aliyetahiri anasifiwa kuwa 'amegusa vyote' katika matini 2. Jazanda ya kinyonga inamaanisha sasa kinembe chake kimeundwa na aliyetahiri anaweza kupata watoto kwani ameruhusiwa kushiriki mapenzi kinyume na yule ambaye hajatahiri. Ikiwa yule ambaye hajatahiri angeshiriki ingekuwa kinyume cha mila na desturi na hivyo huo ni utovu wa heshima. Lakini aliyeshiriki baada ya tohara alichukuliwa kama anatenda jambo la heshima ambalo ameruhusiwa kufanya na wenye uwezo- wale wanaoshiriki katika kufanikisha miviga ya tohara na jamii kwa jumla.

Katika matini 3, aliyetahiri anahesabiwa kuwa atakuwa na heshima kwa watu wote. Waimbaji wanasema:

'Eee mwenzetu awe na heshima
Kwa watu wote ee mwenzetu'

Hii inaashiria kuwa asiyetahiri amekosa heshima. Kama ana heshima, basi si kwa watu wote au hiyo heshima haithaminiwi na jamii. Mojawapo ikiwa heshima rahisi hupatikana katika tohara na mafunzo yaliyomo si vinginevyo.

#### 4.4.3.3 Mikakati ya Kimjadala

Sifa chanya na hasi zilizotolewa zimehalalisha na vifungu kadha vya usemi huu. Matini 1 inadokeza kuwa msichana akitahiri atapata heshima kemkem kutoka kwa jamii hasa kutoka kwa babake. Inasema:

'Naam imekuwa,naam imekuwa

Babake amheshimu, naam imekuwa'

Dai hili linaashiria kuwa ambaye hajatahiri hana heshima kutoka kwa babake na hata jamii nzima. Hii ni kwa sababu katika jamii nyingi za kiAfrika mwanamke aliheshima kuwa wa kiwango cha chini kuliko mwanamume. Hivyo aliyetahiri hutunukiwa heshima kutoka kwa babake ni jambo la muhimu ambalo kila msichana angetamani. Heshima kutoka kwa baba ndicho kilele cha heshima hasa. Hivyo kila msichana akitamani heshima hii angekimbilia ukeketaji kama njia ya kupata tunu hii kubwa.

Katika matini yiyo hiyo, msichana aliyetahiri amepewa jukumu kubwa kabisa la jamii yaani kupata watoto na kuendeleza kizazi. Inasema:

'Apate watoto aendeleze kizazi' (ubeti 5 mshororo 3)

Hili jukumu linaambatana na heshima kubwa. Hivyo, usemi huu umeashiria kuwa aliyetahiri amepewa heshima kuu na jamii. Aidha, inathibitisha imani kuwa ambaye hajatahiri hana heshima. Hii ni kwa sababu hajapewa tunu hii na jamii. Mng'ang'anio wa heshima kutoka kwa jamii, hasa ile inayodunisha mwanamke ungemmotisha msichana kukeketwa.

Katika matini 6, ubeti1, mshororo1, usemi huo umemhesabu aliyetahiri kuwa aliyebarikiwa. Unasema:

'Mtenge mama aliyebarikiwa

Mimi sijabarikiwa nione kifungua mimba'

Kupata baraka hasa ya watoto ni heshima kubwa ambayo hasa ni nyanja ya waliotahiri inavyodhihirika kutoka usemi huu. Hivyo katika harakati za kukazania baraka na heshima inayoambatana, wasichana katika jamii hukimbilia ukeketaji.

### 4.4.4 Kutukuza Utamaduni

Mada hii imechukua nafasi kubwa hasa katika utambulisho wa jamii katika matini zilizochanganuliwa. Utambulisho huo pia umechanganuliwa kwa kutumia mikakati mitatu ya usemi iliyodokezwa na Wodak na Meyer.

#### 4.4.4.1 Unominoshaji

Ukeketaji ilikuwa njia mojawapo ya watu kujitambulisha na jamii, hivi kwamba aliyeasi anahesabiwa katika kikundi cha wale wanaodunisha utamaduni. Haya yanajitokeza katika matini kadhaa zilizochanganuliwa:

Matini 1, ubeti 1, mshororo 3 inamfafanua aliyekeketwa kuwa na jukumu la kupata watoto na kuendeleza kizazi:

'Apate watoto aendeleze kizazi, naam imekuwa'

Kifungu hiki kinaonyesha kuwa ametambuliwa na wale wanaotukuza utamaduni kwani ametwikwa majukumu makubwa ya kuendeleza kizazi. Majukumu ambayo hayajatwikwa ambaye hajatahiri.

Matini 3, aliyetahiri anatambulishwa kama 'mwenzao' na wale ambao wanashiriki katika uimbaji. Wanaimba:

'Ee mwenzetu tunapokuja tukiwa na vita'

Hii inamaanisha kuwa ambaye hajatahiri si mwenzao. Aidha, wanajisifu kuwa katika kikundi chao ambacho wamemkaribisha aliyetahiri. Wamo vitani, na vita hivyo ni vya kutetea mila na desturi za jamii. Hivyo wao wamo katika kikundi kinachotukuza utamaduni ambacho ni bora. Hivyo aliyeasi tohara ni mtoro asiyekuza utamaduni wa jamii.

Katika matini 5, kuna dhana ya shangwe kwa watu wote kwa sababu ya hatua ya wazazi wa mtahiriwa na hata mtahiriwa mwenyewe kuteua jambo bora la kushiriki tohara. Waimbaji wanawasifia wazazi wa mtahiriwa na mtahiriwa mwenyewe. Bila shaka jambo ambalo jamii nzima inalisifia na kulishangilia ni jambo ambalo linatukuza na kukuza utamaduni. Hivyo, mtahiriwa amejitambulisha na kikundi cha wale wanaotukuza utamaduni. Vinginevyo, asiyetahiri amejitambulisha na wale wasiokuza utamaduni wa jamii husika.

Katika matini 6, aliyetahiri anatambulishwa kama mama aliyebarikiwa. Kifungu katika matini hiyo kinasema:

'Mtenge mama aliyebarikiwa'

Hii inaashiria kuwa aliyetahiri sasa amekuwa katika kikundi cha waliobarikiwa. Hii inamaanisha kuwa baraka hizi hutokana na hatua ya kuamua kushiriki tohara. Anayekataa kushiriki tohara anajitambulisha na kikundi ambacho hakipati baraka za jamii. Ikiwa aliyetahiri anabarikiwa, basi ni ithibati tosha kuwa ametukuza utamaduni wa jamii, hivyo, anapongezwa kwa kufanya hivyo. Hivyo anazawadiwa kwa kuchukua hatua njema ya kudumisha utamaduni wa jamii husika.

#### 4.4.4.2 Mikakati ya Uvumishaji

Sifa chanya na hasi zimetwikwa wanaoshiriki na wanaojitenga na tohara katika hali ya kutukuza utamaduni. Katika matini 1, aliyetahiri anaitwa 'msichana mzuri' badala ya 'kisichana'. Yeye amapewa sifa ambazo zilihusishwa na wasichana wakubwa waliobaleghe – kama vile kuunda na kulinda familia, kupata watoto na kushiriki katika miviga ya watu wazima. Ndiposa wanaimba:

'Amekuwa mke wa wavulana, naam imekuwa
Wanaume wamchukue, naam imekuwa'

Hivyo tohara ilihusishwa na msichana kupewa majukumu mapya na hadhi mpya kinyume na asiyetahiri. Haya yalikuwa kama tunu kwa kutukuza utamaduni wa jamii. Kwingineko, katika matini yiyo hiyo, waimbaji wanaidunisha hali yake ya zamani kabla ya tohara. Kifungu kinasema:

'Alikuwa kisichana
Alikuwa mke wa vivulana'

Hizi ni sifa hasi ambazo zinamtambulisha ambaye hajatahiri. Hii ni kwa sababu kama angebaki 'kisichana' na 'mke wa vivulana' basi hangepewa majukumu mapya kama vile; kuolewa, kupata watoto na kuendeleza kizazi. Hii inaashiria kuwa asiyetahiri hakutukuza utamaduni. Hadhi hii mpya aliyotwikwa aliyetahiri iliwafanya wengi kukazania tohara ili nao washiriki katika kutukuza utamaduni.

Sifa chanya pia zinamulikiwa katika matini 3, ambapo aliyetahiri anasifiwa kuwa:

'Amekuwa msichana awezaye kuoleka,
Apewe heshima na watu wote'

Hizi ni sifa anapewa kwa kuwa ameshiriki tohara na hivyo kutukuza utamaduni. Hivi kwamba anayeasi tohara huwa hapati sifa hizi chanya na hivyo anatambulishwa na kikundi kinachodunisha utamaduni. Hali hii inawapa wasichana motisha wang'ang'anie tohara ili nao wasifiwe na wapewe hadhi mpya kwa kutukuza utamaduni.

#### 4.4.4.3 Mikakati ya Kimjadala

Sifa chanya na hasi kuhusu kutukuza zimehalalishwa katika matini kadhaa; Matini 1, ubeti 7, mshororo 3 wanasema:

'Amefanya vizuri'

Hapa waimbaji wanamsifu aliyetahiri kuwa amefanya vizuri. Mtu hapewi sifa nzuri kama hajafanya jambo chema. Washiriki katika usemi huu wanamsifu kwa vile amejitambulisha na wale walio waaminifu katika jamii katika kuhifadhi na kutunza utamaduni. Hivi kwamba ambaye hajashiriki tohara hapewi sifa hizo. Hii ni kwa sababu hajachangia kutukuza mila na desturi za jamii.

Katika matini 7, kiitikio kinasema:

'Shangazi amelima barabarani

Asalimiwe na wapita njia na wasafiri'

Aliyetahiri anaitwa 'shangazi', jina ambalo ni la heshima. Hivyo, yeye amekuwa mtu wa kuheshimiwa baada ya tohara. Aidha, wanadai wamuache alime ili asalimiwe na watu, kumaanisha amepata majukumu mapya ambayo kwayo utamaduni utatukuzwa na kukuzwa. Majukumu hayo ni kushiriki kilimo na kutangamana na wengine wenye hadhi katika shughuli za siku na hata za kipekee zinazohitaji watu wa kikundi chake.

Isitoshe, katika matini 10 anatukuzwa ambaye ni shupavu katika tohara na hivyo anaambiwa ahifadhi siri za miviga yote ya tohara. Anaambiwa kuwa hiki ndicho kitamtambulisha na kikundi cha wenye kukuza utamaduni. Kwingineko, aliyetoboa siri analaaniwa kwa kuambiwa atarajie adhabu ya kifo na wale wa aila yake. Hii itakuwa adhabu kwa kutotukuza utamaduni.

### 4.4.5 Ukarimu

Kujitambulisha na ukarimu kumeshughulikiwa katika matini zilizochanganuliwa. Mikakati mitatu ya lugha imezingatiwa, yaani; Unominoshaji, Uvumishaji na Kimjadala.

#### 4.4.5.1 Mikakati ya Unominoshaji

Katika matini 3, ubeti 3, waimbaji wanauliza mzazi wa mtahiriwa ikiwa amepika vyakula watakavyovila. Wanamwelezea mzazi huyo kuwa wamo njiani kuvila vyakula hivyo kama amevipika. Wanasema:

'Ee mwenzetu, umepika vyakula

Tunakuja kula, ee mwenzetu'

Hapa mzazi wa mtahiriwa ametambulishwa kuwa 'mwenzao' kwa sababu: Amekubali kutahiri msichana wake kama wao na pia kuwaandalia vyakula ambavyo watavila kwa minajili ya

sherehe hii. Kwa mintarafu ya kifungu hiki ni wazi kuwa mzazi wa mtahiriwa ametambulishwa na ukarimu. Vinginevyo, aliyekataa kutahiri wasichana wake alichukuliwa kuwa bahili- hataki kuwalisha wanajamii.

Katika matini 5, waimbaji wanamwomba mzazi wa mtahiriwa vyakula wakidai kuwa watu wote katika jamii wamekubali avitoe. Sababu ni kuwa vya bahili ni mtoto hutoa, wanasema. Kwa mfano, katika kifungu kifuatacho wanasema:

'Vya bahili utupe, chai ya moto tupe

Mtoto amewezesha tupe, chai ya moto tupe'

Hapa wanaashiria kuwa mtoto kupitia tohara huendeleza maadili ya ukarimu katika jamii. Hii ni kwa sababu wazazi walio wachoyo walilazimika kutoa vyakula kwa wanajamii kwani sherehe za tohara zilihusisha shangwe na mlo ambavyo vilishirikisha jamii nzima. Hivyo basi, mzazi aliyeasi tohara kwa watoto wake anahesabiwa kuwa mchoyo, ilhali aliyetahiri wasichana wake alitambulishwa kuwa mkarimu. Ukarimu ukiwa ni sifa ambayo kila mwanajamii angetamani atambulishwe nayo. Hivyo kila mmoja aling'ang'ania utambulisho huu kupitia kwa kutahiri watoto wao kimila. Katika matini 6, ubeti 3, pia dhana hii ya ukarimu imeangaziwa wakiihusisha sifa hii na tohara.

#### 4.4.5.2 Mikakati ya Uvumishaji

Sifa chanya na hasi zimechanganuliwa hasa tukiegemea sifa ya ukarimu. Katika matini 5, waimbaji wamesema katika kiitikio kuwa:

'chai moto tupe'

Kifungu hiki kinadokeza kuwa mzazi anayetahiri msichana wake ana sifa ya kutoa vyakula kwa wingi hivi kwamba vinawafanya washiriki wale kuzidi kiasi. Hii ni sifa ya ukarimu inayokuzwa kwa wazazi wanaotahiri wasichana wao. Hivyo ilikisiwa kuwa anayekataa kutahiri wasichana wake ni mchoyo. Na uchoyo ulichukuliwa kuwa sifa hasi ambayo ilishtumiwa na jamii.

Katika matini 6, ubeti 2, wanasema:

'Ukiombwa mboga hutoi, ni mtoto ametupa

Ukiombwa vidogo huvitoi, ni mtoto ametupa.'

Kifungu hicho kinaashiria kuwa tohara ya watoto ilikuwa njia mojawapo ya kufunza watu wachoyo katika jamii maadili ya ukarimu. Ndiposa wamedokeza kuwa wachoyo wakiombwa hata mboga au vyakula vidogo hawatoi. Lakini, kwa sababu ya tohara ya watoto wao,

wameshurutika kutoa vyakula na kujumuika na wengine. Hivyo kwa njia ya tohara, wazazi hata watahiriwa wanafunzwa sifa chanya ya ukarimu na kuondoa sifa hasi ya ubahili. Ili kukubalika katika jamii, kila mzazi aling'ang'ania kujitambulisha na sifa chanya ya ukarimu, hivyo kutahiri wasichana wake, kwani hiyo ndiyo fursa ya pekee ya kuthibitisha ukarimu wake.

#### 4.4.5.3 Mikakati ya Kimjadala

Sifa chanya na hasi zimechanganuliwa katika matini kadhaa kwa jinsi ya kimjadala katika harakati za kuhalalisha sifa hizi za utambulisho. Katika matini 3, ubeti 2, waimbaji wanasema:

'Ee mwenzetu, umepika chakula,
Tunakuja kula, ee mwenzetu.'

Kifungu hiki kinahalalisha sifa chanya ya ukarimu kwa mzazi wa aliyetahiri kwa kukubali chakula ambacho amepika. Ndiposa wanamwalika mzazi katika mshororo wa pili kuwa watakuja kula chakula chake. Na pia wanamsifia kuwa yeye sasa ni 'mwenzao'. Kisha na maana amekuwa wa kikundi chao, kikundi cha wakarimu. Hatua aliyoichukua ya kutahiri msichana wake na baadaye kuwapa washiriki vyakula ni kukua kwa mzazi husika kiukarimu kwani amevuka kutoka uchoyoni hadi ukarimuni.

Katika matini 5, ubeti 2, mshororo 1 na 3, waimbaji wanasema:

'Leo zote tufurahie, chai moto tupe
Zote tushangilie chai moto tupe.'

Kuna furaha katika ukarimu ambao hasa hukuzwa na sherehe za tohara ambapo wazazi wa watahiriwa wangetoa vyakula. Hivyo kwa kuwa na sifa hii chanya ya ukarimu, washiriki wanasema ni heri wote washangilie hali hii. Vinginevyo, asiyetahiri wasichana wake, hivyo asiyetoa vyakula ni mchoyo. Hivyo basi, kila mmoja aling'ang'ania ajitambulishe na sifa hii ya ukarimu hivyo kukuza ukeketaji.

### 4.5 Upambanuzi wa Athari za Lugha Katika Ukeketaji

Katika kuchanganua athari za lugha katika ukeketaji hatua ya tatu ya nadharia ya Uchanganuzi Hakiki ya Usemi; Upambanuzi, imetumiwa. Katika sehemu hii tumeeleza vile michakato ya Maingiliano na Tendo la Jamii inavyoingiliana. Tumechunguza muktadha wa nyimbo katika ukeketaji na itikadi za jamii zinazojitokeza katika nyimbo za ukeketaji na

zinavyokuzwa kupitia lugha inayotumika katika nyimbo hizi na mchango wake katika kukuza asasi hii ya ukeketaji.

### 4.5.1 Muktadha wa Nyimbo Katika Ukeketaji

Tohara ilikuwa jambo muhimu sana katika jamii. Ilikuwa kama daraja la kuvusha watoto wasichana hadi utu uzima. Kama shughuli zingine muhimu katika jamii nyimbo ziliambatana na sherehe za tohara. Matarajio ya jamii kwa watahiriwa yaliwasilishwa kwao kwa njia ya nyimbo. Nyimbo ziliimbwa kuwafahamisha wamekuwa watu wakubwa na tayari kuchukua majukumu makubwa katika jamii kama vile kuolewa na kuheshimiwa. Nyimbo hizo zilikuwa kama kifaa cha kuwaelimisha waliotahiri. Isitoshe, nyimbo hizo zilibainisha majukumu kwa minajili ya jinsia. Pia nyimbo hizi ziliwafunza maadili mema kama vile uvumilivu.

Nyimbo huibua hisia na kuwapa changamoto wale ambao hawajatahiri kungojea siku ya kutahiri kwa hamu kuu. Kwa hivyo si ajabu kuwa nyimbo za tohara zilikuwa na vivumishi nomino na jazanda zilizotukuza waliotahiri ilhali zinatweza waliokosa kutahiri.

Nyimbo za nyiso katika jamii ya Abagusii ni fupi na sahili. Zinaambatana na kunengua viuno na kushangilia kwa vifijo na miluzi. Aidha, zana za muziki kama vile ngoma vilishirikishwa ili kuleta uhondo zaidi katika nyimbo. Isitoshe, watahiriwa walipokuwa wakizindikizwa nyumbani, kushangilia kwa sauti kubwa na kwa furaha kubwa pamoja na kurukaruka vilihusishwa na nyimbo hizi. Kwa kawaida, waimbaji wanabeba matawi kama ishara ya furaha na hata wengine hujipamba kwa maua na matawi mbalimbali. Rangi ya kijani kibichi ya matawi yaliyobebwa yanaashiria uhai ilhali maua hasa yale ya kimanjano yanaashiria tumaini katika maisha ya Abagusii, hasa katika mazao ya shambani. Hivyo, kuashiria kuwa hata mtahiriwa ana tumaini la kuchangia katika maendeleo ya jamii.

Nyimbo mbalimbali ziliimbwa kulingana na hatua mbalimbali za mchakato wa shughuli za ukeketaji. Kila wimbo ulisheheni maudhui yanayoafiki mafunzo yanayolengwa katika hatua husika. Mbinu ya takriri imetumiwa kwa wingi ili kukuza uhifadhi wa nyimbo katika tafakuri za waimbaji na hadhira yao kando na kusisitiza ujumbe teule unaotiliwa mkazo na jamii husika.

Hata hivyo, hakuna la mno katika tohara yenyewe, ila kudumisha mila na desturi za jamii. Mila ambazo humshikanisha mtahiriwa na jamii yake. Ilieleweka kuwa anayeasi mila hii ni kama kuasi utamaduni wake na hata jamii yake. Ndiposa, mafunzo yatolewayo katika vikao

vya kulaani ukeketaji kwa kutafuta njia zingine za kuvusha wasichana kutoka utotoni hadi utu uzima yamegonga mwamba.

Nyimbo kama kifaa muhimu cha kuelimisha jamii hasa kuhusu tohara zimechanganuliwa ili kuakisi athari zake katika kuendeleza ukeketaji.

### 4.5.2 Athari za Lugha Katika Ukeketaji

Ingawa athari za lugha katika kuendeleza ukeketaji zimeshughulikiwa katika kufafanua madhumuni ya kwanza mawili ya utafiti wetu, tutapambanua athari zingine kwa kuangazia itikadi za Abagusii zinavyokuzwa kupitia lugha na maudhui yanayojitokeza katika matini kumi za ukeketaji tulizokusanya.

#### 4.5.2.1 Ukeketaji Hukuza Uke na Ndoa

Matini hizi kuhusu ukeketaji zilitukuza uke na ndoa. Ukeketaji unahusudiwa kama nyenzo ya kumpa mafunzo kuhusu uke na jinsi ya kuwajibika katika ndoa. Majukumu yaliyoambatana na uke na maisha ya ndoa yalibainishwa kama vile mapenzi, kumlinda mume, kupata na kulea watoto. Majukumu hayakuhusishwa na yule ambaye hajatahiri kwani hawezi kuwajibika kama mke katika ndoa. Hata kuolewa haruhusiwi hadi atahiriwe. Kwa hivyo ilikuwa jambo jema ikiwa ulikuwa katika kikundi cha waliotahiri. Hiyo ndio njia bora ambayo kwayo ungetunukiwa ili jukumu muhimu la kuendeleza kizazi cha jamii. Haya yanajidhihirisha waziwazi katika matini 1, 2, 3, 8 na 10.

Katika matini 1, ubeti 3, mshororo 2 na 3, waimbaji wanadai kuwa sasa wanaume wanaweza kumuoa na apate watoto ili kuendeleza kizazi. Katika matini hii, ni wazi kuwa lugha iliyotumika imetilia mkazo imani kuwa ili kukuza uke na kushiriki asasi ya ndoa ili kuendeleza kizazi sharti ushiriki ukeketaji. Msichana asiyefuata mkondo huu, haruhusiwi kushiriki ndoa na si mwanamke kamili. Ikiwa angeshiriki basi angepata maafa fulani kama vile kutopata watoto au ikiwa angepata wangekufa. Lugha hii ambayo imetumika katika matini hizi inamwogofya msichana anayefikiria kuasi asasi hii, hivyo kuishiriki. Kwa njia hii lugha hii inakuza ukeketaji.

Katika matini 3, ubeti 4, waimbaji wanadai kuwa aliyetahiri amekuwa mwanamke ambaye anaweza kuolewa na kushiriki katika kuendeleza kizazi cha jamii. Wanasema:

'Ee mwenzetu, amekuwa mwanamke
Awezaye kuolewa, ee mwenzetu

Hapa imani hii kuwa ukeketaji hukuza uke na ndoa pia imetiliwa mkazo katika matini hii kupitia lugha hii iliyotumika. Tukizingatia kuwa hadhira ya matini hizi ni wale waliokeketwa na wale ambao hawajakeketwa, ni wazi kuwa ujumbe huu huchangia katika kukuza asasi hii ya ukeketaji katika jamii ya Abagusii.

#### 4.5.2.2 Ukeketaji Hukuza Uvumilivu

Matini hizi kuhusu ukeketaji zilimkuza aliyetahiri kama aliye na maadili mema kama vile uvumilivu. Kwa kuvumilia miviga yote ihusuyo tohara aliyetahiri huwa amekuza maadili ya uvumilivu. Ambaye hajatahiri huhesabiwa kuwa mwoga. Hivyo aliyetahiri ni mvumilivu na hivyo shujaa, kinyume na asiyetahiri ambaye anachukuliwa kuwa mwoga ambaye hawezi kuvumiliwa katika jamii. Haya yanajitokeza katika matini 8 na 9. Katika matini 8, kwa ujumla dhana ya uvumilivu imetiliwa mkazo. Ikizingatiwa kuwa wimbo huu uliimbwa wakati wa mkesha wa mahafali, ulilenga aliyekeketwa awe na ujasiri wa kuvumilia miviga yote iliyobaki ili aje kufaidi manufaa yote ya aliyetahiri. Hii ni kwa sababu wimbo ulimulikia mafunzo ya mila na tamaduni za jamii ambapo uvumilivu ulihitajika ili asije akapata mume duni kwa kutovumilia miviga yote hasa hii ya mwishomwisho.

Aliyekeketwa anahimizwa kuwa asiolewe na mzee bali aolewe na mvulana chipukizi. Haya yangewezekana iwapo angeepuka kulia akiwa jandoni. Ndiposa wanaimba katika ubeti wa 3, mshororo wa 1 na 2:

> 'Nikiolewa na mzee, nikamue kipofu, nimeshangaa
> Nikiolewa na mvulana, nikamue mengi,nimeshangaa

Aidha, katika matini 9, ambao ni wimbo huimbwao mkesha wa mahafali husisitiza nidhamu katika kuhifadhi siri za shughuli zote za ukeketaji. Mtahiriwa aliyejizuia kuhifadhi siri hizi ili asiseme kwa ambao hawajakeketwa angechukuliwa kuwa na uvumilivu na utu uzima. Aliyevumilia hivi angepata baraka zote za jamii kama vile kushiriki ndoa na kupata watoto. Uhifadhi huu ungemsukuma msichana ambaye hajakeketwa kuwa na hamu kubwa ya kutaka kujua siri hizi, hivyo kutamani kukeketwa na kuendeleza asasi hii.

#### 4.5.2.3 Ukeketaji Humpa Heshima na Hadhi Aliyekeketwa

Matini takriban zote zilimuakisi aliyetahiri akiwa mwenye heshima na anayestahili kupewa heshima. Alimulikwa kuwa ameacha mizaha ya kitoto na watoto. Hata wazazi na

wenzake walihimizwa kumheshimu. Anakaribishwa kushiriki yale ambayo wenye heshima wanayashiriki kama vile kuwa na urafiki wa kimapenzi na wavulana chipukizi si watoto tena. Hayo yamedhihirika zaidi katika matini 2, 3, 4 na 6. Katika matini 4, aliyetahiri anasifiwa kuwa yeye ni nyota ya asubuhi ambayo itawamulikia wengine. Hapa amepewa heshima kubwa ya kuwaongoza wengine katika jamii kwani amepitia awamu zote zinazohitajika katika jamii hasha kuhusiana na hatua ya kumvusha kutoka utotoni hadi utu uzima. Hii inamaanisha kuwa ambaye hajakeketwa hana heshima hii ya kuwa mwangaza wa kuwamulikia wengine kuhusu yapasayo kufanywa katika jamii. Hamu ya msichana kutaka kutunukiwa heshima na hadhi hii ingemsukuma atake kukeketwa hivyo kuuendeleza.

Katika matini 6, ubeti 1, waimbaji wanamuakisi aliyekeketwa kuwa ni mama aliyebarikiwa na aweza kuolewa na kupata watoto na kwa hayo anashangiliwa sana. Wanasema asiyepitia hatua hii hatabarikiwa. Hamu ya msichana pia kupata watoto katika ndoa kama heshima na hadhi mpya kwa aliyetahiri inamfanya ambaye hajatahiri akazanie asasi hii hivyo kuiendeleza.

Matini pia zinadokeza kuwa aliyeshiriki tohara alipata hadhi kubwa pamoja na majukumu yanayoambatana na hadhi hiyo mpya. Kwa mfano, aliyetahiri aliweza kuitwa msichana badala ya kisichana, angeshirikiana na wavulana wakubwa wala si watoto, angeshiriki kilimo na katika sherehe zote za jamii zilizohitaji wanawake wakubwa. Hivyo, kila mmoja katika jamii alihimizika kutahiriwa ili apate hadhi hii mpya pamoja na majukumu makubwa na mapya.

Haya unajitokeza zaidi katika matini 1, 3, 4, 6 na 9. Kwa mfano, katika matini 1 , ubeti wa 4, wanasema:

> 'Naam imekuwa, naam imekuwa
> Babake amheshimu, naam imekuwa
> Awe mke mzuri, naam imekuwa.'

Katika usemi huu, aliyekeketwa anaelezwa kuwa na hadhi mpya ya 'mke' si msichana tena. Si mke tu bali mke mzuri. Isitoshe, katika usemi uu huu anahimizwa amheshimu aliyekeketwa. Hiyo heshima atakayopewa na baba asingepewa kama si hatua ya ujasiri ya kukeketwa. Kwa hivyo, hadhi hii kubwa ya kuitwa 'mke mzuri', kupewa heshima na baba na majukumu mengine mengi yanakuwa kichocheo cha kutamani kukeketwa hivyo kuukuza.

#### 4.5.2.4 Ukeketaji Hukuza Utamaduni

Ujumbe katika matini hizi unaangazia nyimbo kama njia ya kukuza mila na desturi za jamii. Zilihakikisha kuwa anayetahiri amefuata kanuni za jamii hivyo kuzihifadhi na kuzikuza. Hivi kwamba anayeasi tohara huwa ameshusha utamaduni. Hivyo yeye anachukuliwa kuwa mwasi na anayetakiwa kutengwa na wengine katika jamii. Hivyo mshiriki katika miviga ya tohara anahimizwa kuhifadhi siri za miviga hii. Aliyeenda kinyume na kiapo cha kuhifadhi siri, adhabu yake ingekuwa kifo; kifo chake mwenyewe au mume wake hata watu wa familia yake. Hivo njia nyingine ya kutukuza utamaduni ni kuhifadhi siri ya miviga ya tohara. Isitoshe, aliyetahiri alihesabiwa amefungamanishwa na mababu wa jamii. Haya yanajitokeza katika matini ya 10.

Kwa mfano, katika matini 10, ubeti 4, waimbaji wanasema kuwa atakayesema siri za tohara atalaaniwa kwa njia mbalimbali kama vile kifo chake au cha wale wa familia yake. Baadhi ya mafunzo waliyopewa yalihusu amali mahususi za jamii yao ambazo hazikutakiwa zijulikane na wale wasio wa jamii hiyo. Kwa aliyekeketwa anahesabiwa mtu mzima anapewa mafunzo haya na kuhimizwa asiyatoe kwa wale wasio wa jamii au watoto katika jamii. Msichana ambaye hajatahiri anahesabiwa mtoto au asiye wa jamii. Shughuli yenyewe ya tohara ilikuwa njia mojawapo ya kuendeleza utamaduni wa Abagusii. Hivi kwamba aliyepuuza asasi hii angechukuliwa kuwa mwasi wa mila na utamaduni wa jamii ambaye angepata laana. Ndiposa hakutakiwa apewe siri za jamii. Waimbaji wasema:

"Ukisema siri zetu, ulaaniwe
Watoto wako wafe, ulaaniwe
Mume wako afe, ulaaniwe
Mavyaa wako afe, ulaaniwe.'

Hali hii ilimsukuma msichana ambaye hajatahiri akimbilie tohara ili ajue mafunzo muhimu ya jamii na achangie katika kuukuza utamaduni asije akaitwa mwasi katika jamii.

#### 4.5.2.5 Ukeketaji Hukuza Maadili ya Ukarimu

Sifa hii pia inajitokeza katika matini kadhaa. Kushiriki tohara kulihusishwa na sifa ya ukarimu: kwa wazazi wa watahiriwa na watahiriwa. Hivi kwamba mzazi ambaye hakutahiri watoto wake alichukuliwa kuwa bahili; ambaye hataki kuwapa wanajamii chakula. Hivyo kila mmoja wa wazazi wa vijana alitamani kushirikisha watoto tohara ili waitwe wakarimu, la sivyo

waitwe bahili. Haya yanajitokeza katika matini 3, 5 na 6. Katika matini 6, ubeti wa 3, mzazi wa mtahiriwa ashangiliwa kuwa ameacha ubahili na kuwa mkarimu kwa kumtahiri msichana wake kwani sasa imembidi kuwalisha waliohudhuria kushiriki na kushuhudia shughuli hii. Wanasema:

'Cha bahili ni mtoto ametupa

Ukiombwa mboga hutoi, ni mtoto ametupa

Akashangilia aririri

Asiyependelea, asiyelaani

Huu ni mfano wa vile kila mzazi angetazamia kumkeketa msichana wake asije akabandikwa jina bahili. Katika juhudi hizi ukeketaji utakuwa unaendelezwa.

**4.6 Hitimisho**

Katika sura hii, tumechanganua matini tukiegemea madhumuni yetu matatu ya utafiti na nadharia ya utafiti tulioiteua (Uchanganuzi Hakiki wa Usemi). Tumefafanua sifa nne za lugha za matini wa utafiti: matumizi ya takriri; vivumishi; nomino na jazanda. Aidha, ufasili wa utambulisho wa jamii unavyojitokeza katika matini za ukeketaji umefanywa.Mikakati mitatu ya lugha iliyodokezwa na Wodak na Meyer (2001:73) ilitumika katika ufasili huu. Mikakati hiyo ni: Unominoshaji, Uvumishaji na Kimjadala. Mikakati hii imesaidia katika kuhalalisha na kuharamisha sifa chanya na sifa hasi zinazopewa waliotahiri na wale bado kutahiri. Utambulisho huu uliegemezwa kwenye mada tano zilizojitokeza katika matini za utafiti: Uke na ndoa; uvumilivu; ukarimu; heshima na hadhi kubwa; na kutukuza utamaduni. Hatimaye, upambanuzi wa athari za lugha katika ukeketaji tukiegemea katika itikadi zinazotokana na mada tano tulizozirejelea hapo juu ambazo zimejengwa katika usemi wa ukeketaji ulifanywa.

## SURA YA TANO

## MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti ametathmini maswala muhimu yaliyoibuka kutokana na utafiti huu. Aidha, amegusia matatizo na ufanisi w utafiti huu. Hatimaye, ametoa mapendekezo kuhusu sehemu zinazohitaji kufanyiwa utafiti zaidi.

### 5.2 Muhtasari na Hitimisho

Katika utafiti huu, tumechanganua usemi katika ukeketaji wa wanawake katika jamii ya Abagusii. Dhamira ya utafiti huu ilikuwa ni kuchunguza sifa mahususi za lugha inayotumiwa katika usemi wa ukeketaji; kutathmini vile utambulisho wa kijamii na mahusiano ya kijamii yanavyojengwa kupitia kwa usemi huu na athari za lugha inayotumiwa katika kuendeleza ukeketaji. Ilidhihirika kwamba, Abagusii hupitisha na kuwarithisha wanajamii amali, imani na itikadi ambazo hudhihirika katika lugha wanayoitumia.

Uchanganuzi wa nyimbo za tohara zilizotumiwa kama matini teule katika usemi huu zilithibitisha ukweli wa nadharia tete ya kwanza iliyodai kwamba lugha inayotumiwa katika usemi wa ukeketaji ina sifa mahususi. Ilidhihirika kuwa, lugha inayotumiwa katika usemi huu imejaa nomino na vivumishi vilivyomkuza na kumtukuza aliyetahiri huku vikimtweza asiyetahiri. Aidha, matumizi ya takriri na jazanda katika usemi huu yamesaidia kutilia mkazo mafunzo yaliyoenzi ukeketaji hivyo kuwachochea wasichana wengi kupapia ukeketaji.

Nadharia tete ya pili pia ilithibitishwa katika uchanganuzi wetu ambayo ilidai kuwa asasi ya ukeketaji wa wanawake hujenga utambulisho wa kijamii na mahusiano ambayo hudhihirika katika usemi unaouzunguka. Kupitia kwa mikakati mitatu ya lugha, yaani: unominoshaji, uvumishaji na kimjadala mtafiti alithibitisha ukweli wa nadharia tete hii. Kupitia kwa mikakati hii waliotahiri walijenga utambulisho na uanachama waliouenzi huku wakibagua na kushusha wasiotahiri. Walijipa sifa chanya na kuwapa wasiotahiri sifa finyu huku wakihalalisha sifa hizi kupitia kwa lugha iliyotumiwa katika usemi huu.

Nadhari tete ya tatu pia inathibitishwa katika uchanganuzi wetu, ambapo tuligundua kuwa lugha inayotumiwa huchangia katika kuendeleza ukeketaji. Hii ni kwa sababu, lugha inayotumiwa katika usemi huu wa ukeketaji inamtukuza anayetahiri huku ikimdunisha asiyetahiri. Lugha hii imekuwa msingi wa imani na amali za jamii, hasa imani kuhusu umuhimu

wa ukeketaji ambayo imeshika mizizi kiasi cha kuwa vigumu kuibomoa kwani imesheheni sehemu ya utamaduni wa Abagusii.

Hata hivyo, matokeo ya utafiti yalifikiwa kupitia kwa nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi iliyoongoza utafiti huu licha ya matatizo tutakayoeleza katika 5.3. Ni muhimu kuelewa kwamba, madhumuni yetu ya utafiti yameafikiwa na nadharia tete zimethibitishwa kuwa kweli.

## 5.3 Matatizo Yaliyomkabili Mtafiti

Ilikuwa vigumu kupata nyimbo zilizohitajika kama matini ya uchanganuzi wetu. Hii ni kwa sababu ilidhihirika kwamba wanawake wa maeneo tofauti walikuwa na beti kadhaa za wimbo uleule. Aidha, nyimbo za kidini zimejipenyeza katika usemi wa ukeketaji hivi kwamba imani na amali za dini ya Kikristo zimefungamanishwa na zile za kitamaduni katika kukuza mila hii.

Changamoto nyingine ilikuwa katika kutafsiri. Deta iliyokusanywa ilikuwa kwa lugha ya Ekegusii. Hii ililazimisha utafsiri ufanywe kama sharti la kazi hii. Baadhi ya dhana tulizozipata zilikosa visawe vyao katika lugha ya Kiswahili. Kwa sababu hii, huenda tulitoa maelezo ambayo hayataibua maana iliyokusudiwa katika muktadha asilia. Hata hivyo, mtafiti alijaribu kuleta uwiano kati ya lugha chanzi na pokezi kwa kufanya mahojiano ya kina kuhusu maswala na msamiati tata kwa akina mama teule.

## 5.4 Mapendekezo

Kuna mambo muhimu yaliyobainika kutokana na utafiti huu. Kwanza, mtafiti aligundua kwamba tanzu za fasihi simulizi kama vile ngano, vitendawili na methali zinahitaji kufanyiwa utafiti kuchanganua zinavyochangia katika kuendeleza asasi hii ya ukeketaji.

Vilevile, mtafiti aligundua kwamba kuna imani zilizoibuliwa na baadhi ya nyimbo ambazo zimepitwa na wakati. Kwa hivyo, wanajamii wa kisasa wa wajibu wa kutunga nyimbo zinazoafiki utambulisho wa kijamii wa kisasa na kuimarisha vita dhidi ya ukeketaji na kubadilisha polepole imani zihusuzo mila hii.

Aidha, serikali kupitia kwa Wizara ya Elimu inapaswa kuhakikisha kuwa, mtalaa wa masomo umebadilishwa ili kujumuisha mada zihusuzo madhara ya ukeketaji kwa wasichana katika jamii.

Isitoshe, serikali kupitia vyombo vyake vya utawala, inatakikana kudumisha sera ya kupiga marufuku mila ya ukeketaji wa wasichana katika jamii. Hatimaye, wahubiri na wanaotetea haki za wanawake wanahimizwa kushirikiana katika kuelimisha jamii kuhusu madhara ya ukeketaji huku wakilenga kugusa na kubadilisha imani zilizoko ambazo zimeshika mizizi.

# MAREJELEO


Ali, A.M. (2003). *A study of Factors Perpetuating Infibulation Among Somali- Muslims in Mandera District*. M.A Thesis: Kenyatta University

Assad, M.B. (1980). "Female Circumcision in Egypt: Social Implications, Current Research and Prospects for Change" in *Studies in Family Planning*, II (1), 3-16.

Backlander, C. (n.d). Female Genital Mutilation in Kenya. Retrieved March 25, 2010, from http: // womenontherun.se/node/42

Brown, G. and G. Yule (1993). *Discourse Analysis*. Cambridge: CUP.

Burton, G. (1997). *More Than Meets the Eye: An Introduction to Media Studies*. London: Arnold.

Castledine, J. (n.d). Female Genital Mutilation: An issue of Cultural Relativism or Human Rights? Retrieved April 6, 2010, from http:// www.mtholyoke.edu/acad./intrel/jc.htm

Delano, E. (1988). "Female Circumcision" in *A Guide to Family Planning*. Nairobi: E.A.E.P.

Elmi, M.Y. (2003). *Female Genital Mutilation: Health Problems Among the Somali Community in Garissa Town, Kenya*. M.A Thesis: Kenyatta University.

Fairclough, N. (ed.). (1992). *Critical Language Awareness*. Essex: Longman.

Fairclough, N. (1992). *Discourse and Social Change*. London: Polity Press.

Fairclough, N. (1989). *Language and Power*. Harlow: Longman.

Forward (n.d). Kenya- Mobilising men against female genital mutilation in Kenya. Retrieved March25, 2010, from http://www.forwarduk.org.uk/what-we-do/past-programmes/kenya.

Haig, E. (2001). "A study of the Application of Critical Discourse Analysis to Ecolinguistic and Teaching of Ecoliteracy, *Studies in Language and Culture*. Nagoa University, 22: 205-226.

Katumba, R. (1990, September). "Kenyan Elders Defend Circumcision". *Development forum*, 17.

Kenyatta, J. (1938). *Facing Mount Kenya: The Tribal Life of the Kikuyu*. Seeker and Warburg: London.

Laura, R., Mohamud, A. and Ali, N. (n.d). Female Genital Mutilation-The Facts. Retrieved April 6, 2010, from http:// www. path.org/files/FGM- The Facts.htm

Lightfoot- Klein, H. (1989). "The Sexual Experience and Marital Adjustment of Genitally Circumcised and Infibulated Females in Sudan", *The Journal of Sex Research*, 26 (3), 375-392.

Lightfoot- Klein, H. (1989). *Prisoners of Ritual: An Odyssey into Female Genital Circumcision in Africa.* Hoxworth Press: New York.

Lull, J. (1996). *Media Communication and Culture: A global Approach.* Cambridge: Polity Press.

Mbugua, I. (1997). Ending the Mutilation, *People and the Planet,* 6, (1), 19.

Mokaya, D.M. (2007). *Female Circumcision Amongst the Abagusii people in Kenya.* Kendu Bay: AHPH.

Mose, G.B. (1997). *The Abagusii Female Circumcision and its Impact on Women's Role in Society.* M.A Thesis: Kenyatta University.

Mugenda, O. and A. Mugenda. (1999). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches.* Nairobi: Acts Press.

Nyang'era, N.K. (1999). *The Making of Man and Woman under Abagusii Customary Laws.* Kisii: Dal-rich Printers.

Nyansera, B.K. (1994). *Female Circumcision: Its Persistence Among the Abagusii of Kenya.* M.A Thesis: University of Nairobi.

Ochieng', O. (2005, February 8). FGM in Kenya : Outlawed, not Eradicated. Retrieved March 25, 2010, from http: // www. feminist. com/news/vaw 39.hmtl

Shiffrin, D. (1994). *Approaches to Discourse*. Cambridge: Polity Press.

Sonkoyo, L. (2005, December 1). "Men have a place in FGM War" in *The Standard*, pp.13.

Toubia, N. (1993). *Female Genital Mutilation- A call for Global Action.* Rainbo: New York.

UNICEF. (2005). *Female Genital Mutilation: A statistical Exploration.* New York: UNICEF.

Van Dijk, T. (1997). *Discourse as Social Interaction.* London: Sage Publications.

Wallace, C. (1992). "Critical Awareness in the EFL Classroom" in Fairclough, N. (ed) *Critical Language Awareness*. Essex: Longman.

Wodak, R. and M. Meyer. (eds) (2001). *Methods of Critical Discourse Analysis: Introduction Qualitative Methods.* London: Sage Publications.

## KIAMBATISHO A

## MATINI 1

## *OYAYE OYEE*

1. *Oyaye oyee- oyaye oyee x 2-* Naam imekuwa- Naam imekuwa x 2

   *Itaba buya, itaba gwancha, oyaye oyee* – Itika vizuri, itika kwa kukubali, naam imekuwa

   *Itaba buya, ntonaneire, oyaye oyee-* Itika vizuri, tumekubalika, naam imekuwa.

2. *Oyaye oyee-oyaye oyee x 2-* Naam imekuwa, naam imekuwa

   *Orenge egesagane, oyaye oyee-* Alikuwa kisichana, naam imekuwa

   *Obeire omoiseke omosera,oyaye oyee-*Amekuwa msichana mzuri, naam imekuwa.

3. *Oyaye oyee-oyaye oyee x 2* – Naam imekuwa, naam imekuwa

   *Orenge mokabaisia, oyaye oyee-* Alikuwa mke wa vivulana, naam imekuwa

   *Obeire mokabamura, oyaye oyee-* Amekuwa mke wa wavulana, naam imekuwa.

4. *Oyaye oyee – oyaye oyee x 2-* Naam imekuwa, naam imekuwa x 2

   *Ise omosikee, oyaye oyee x 2-* Babake amheshimu, naam imekuwa

   *Abe mokungu muya, oyaye oyee* – Awe mke mzuri, naam imekuwa.

5. *Oyaye oyee- oyaye oyee x2* – Naam imekuwa, naam imekuwa

   *Abamura bamoire, oyaye oyee,* Wanaume wamuoe, naam imekuwa

   *Anyore abana arosie egesaku, oyaye oyee-* Apate watoto aendeleze kizazi, naam imekuwa.

6. *Oyaye oyee- oyaye oyee* – Naam imekuwa, naam imekuwa

   *Goko okorire buya, oyaye oyee-*Msimamizi wake amefanya vizuri, naam imekuwa

   *Otigire egosorio, oyaye oyee-* Ameacha mizaha, naam imekuwa.

7. *Oyaye oyee- oyaye oyee-* Naam imekuwa, naam imekuwa

   *Simbore oito aru rogoro, oyaye oyee-* Wimbo wetu watoka juu, naam imekuwa

   *Omwana okorire buya, oyaye oyee-* Mtoto amefanya vizuri, naam imekuwa.

## KIAMBATISHO B

## MATINI 2

## *KUNA MOYARE*

1. *Gwakunire enkuna, kuna x 2*- Umegusa kitu, gusa x 2
   *Kuna moyare ee baba, kuna*- Gusa mwenzangu uu mama, gusa.

2. *Nakunire enkuna, kuna x 2*- Nimegusa kitu, gusa x 2
   *Kuna moyare ee baba, kuna x 2*- Gusa mwenzangu uu mama, gusa.

3. *Gwakunire egoto, kuna x 2*- Umegusa uchafu, gusa x 2
   *Kuna moyare ee baba, kuna x 2*- Gusa mwenzangu uu mama, gusa.

4. *Nakunire enyambu, kuna x 2*- Nimegusa kinyonga, gusa x 2
   *Kuna moyare ee baba, kuna x 2*- Gusa mwenzangu uu mama, gusa.

5. *Kuna onkuneranie, kuna x 2*- Gusa nami unigusie, gusa x 2
   *Kuna moyare ee baba, kuna x 2*- Gusa mwenzangu uu mama, gusa.

6. *Nakunire bionsi, kuna x 2*- Nimegusa vyote, gusa x 2
   *Kuna moyare ee baba, kuna x 2*- Gusa mwenzangu uu mama, gusa.

7. *Nakunire ekoko, kuna x 2*- Nimegusa taka , gusa x 2
   *Kuna moyare ee baba, kuna x 2*- Gusa mwenzangu uu mama, gusa.

**KIAMBATISHO C**

**MATINI 3**

***EE WAMAYA***

1. *Ee wamaya x 4-* Ee wenzetu x 4

   *Ee wamaya ng,ai togochia ?* – Ee wenzetu, twaenda wapi?

   *Sobo omware togochia, ee wamaya x 2-* Kwa mtahiririwa ndiko twaenda, ee wenzetu x 2.

2. *Ee wamaya kwarosirie endagera?* – Ee mwenzetu umepika vyakula

   *Togocha koria, ee wamaya x 2-* Tunakuja kula, ee mwenzetu x 2

3. *Ee wamaya, ekero togocha-* Ee mwenzetu, tunapokuja,

   *Tore n'esegi, ee wamaya x 2-* Tukiwa na vita, ee mwenzetu x 2.

4. *Ee wamaya, obeire omoiseke-* Ee mwenzetu, amekuwa msichana

   *Oragende bwoye, ee wamaya-* Awezaye kuolewa, ee mwenzetu x 2.

5. *Ee wamaya, atware amasikani-* Ee mwenzetu, awe na heshima,

   *Ase abanto bonsi, ee wamaya-* Kwa watu wote, ee mwenzetu x 2.

6. *Ee wamaya, Moraa nchwo bwango-* Ee mwenzetu, Moraa njoo haraka

   *Nchwo bwango tokorore, ee wamaya-* Njoo haraka ili tukuone, ee mwenzetu x 2

7. *Ee wamaya, Moraa nchara tore-* Ee mwenzetu, Moraa tuna njaa,

   *Moraa twomire, Moraa nki obwate, ee wamaya-* Moraa tumekauka, Moraa una nini, ee mwenzetu x 2

**KIAMBATISHO D**

**MATINI 4**

***EYAROGORO***

1. *Eyarogoro x 4, rogoro ndonga rogondereria*- Macheo x 4, Macheo huja polepole
   *Eyarogoro x 2, rogoro nyacha eite bokingite, eyarogoro*- Macheo x 2 Macheo, yaja itoe baridi, macheo x2

2. *Mbwanagokia mongesa etatongeti, eyarogoro x 2*- Hakujawahi kucha jua lisipochomoza,
   *Rogoro ndonga rogondereria eyarogoro x 2 rogoro nyacha eite bokingite, eyarogoro*-
   Macheo ya polepole, Macheo x 2 Macheo, yaja itoe baridi, macheo x 2.

3. *Koroche mongesa gegotonga, eyarogoro x 2*- Ukiona jua likichomoza, macheo x 2
   *Rogoro ndonga rogondereria eyarogoro x 2 rogoro nyacha eite bokingite, eyarogoro*-
   Macheo ya polepole, Macheo x 2 Macheo, yaja itoe baridi, macheo x 2.

## KIAMBATISHO E

## MATINI 5

## *ECHAE YA MORERO TOE*

1. *Bangina n'abana soa, echae ya morero toe-* Akina mama na watoto ingia, chai moto tupe
   *Nonya mbike igo toe, echae ya morero toe-* Hata vichache chai moto tupe
   *Rero n'ekegeni kiao, echae ya morero toe-* Leo ni sherehe yako, chai moto tupe.

2. *Rero twensi n'omogoko, echae ya morero toe-* Hata vichache tupe, chai moto tupe
   *Nonya ng'akeigo toe, echae ya morero toe-* Hata vichache tupe, chai moto tupe
   *Minto twensi tochenge, echae ya morero toe* – Zote tushangilie, chai moto tupe.

3. *Omogaka Onsongo nabo, echae ya morero toe-*Mzee Onsongo ndio, chai moto tupe
   *Mong'ina Kerubo nabo, echae ya morero toe-* Mama Kerubo ndio, chai moto tupe
   *Bang'ina bancheranire, echae ya morero toe* – Akina mama wamekubali, chai ya moto tupe

4. *Nonya mbike igo toe, echae ya morero toe-* Hata vichache tupe, chai moto tupe.
   *Eki'omogoko toe, echae ya morero toe-* Vya bahili tupe, chai moto tupe
   *Omwana ogerire toe, echae ya morero toe-* Mtoto ndiye amewezesha tupe, chai moto tupe
   *Intwana goika aa, echae ya morero to*e- Hatujawahi fika hapa, chai moto tupe.

## KIAMBATISHO F

## MATINI 6

## *ATUTA BABA*

1. *Atuta baba ere ogoreire x 2* – Mtenge mama aliyebarikiwa x 2
   *Nche tingoreiri ndore omotangi x 2*- Mimi sijabarikiwa nione kifungua mimba
   *Gasamba keiririato aririri*- Akashangilia, aririri
   *Nyamaegerio, nyamasenyente*- Aliyependelewa, asiye laini.

2. *Nosabwa bieni tokobirwa n'omwana ogetoire*- Ukiombwa mboga hutoi, ni mtoto ametupa
   *Nosabwa bike tokobirwa n'omwana ogetoire*- Ukiombwa vichache huvitoi, ni mtoto ametupa
   *Ogasamba keiririato, aririri*- Akashangilia, aririri
   *Nyamaegerio, nyamasenyente*- Aliyependelewa, asiye laini.

3. *Ekio'mogoko n'omwana ogetoire*- Cha bahili ni mtoto ametupa
   *Nosabwa bieni tokobirwa, n'omwana ogetoire*- Ukiombwa mboga hutoi, ni mtoto ametupa
   *Ogasamba keiririato, aririri*- Akashangilia, aririri
   *Nyamaegerio, nyamasenyente*- Aliyependelewa, asiye laini

4. *Sabera baba omwana ankio eberebenche ebene*- Tumwombee mama mtoto ili kesho awepo
   *Nosabwa bike tokobirwa n'omwana ogetoire*- Ukiombwa vichache huvitoi, ni mtoto ametupa
   *Ogasamba keiririato, aririri*- Akashangilia, aririri
   *Nyamaegerio, nyamasenyente*- Aliyependelewa, asiye laini.

**KIAMBATISHO G**

**MATINI 7**

***ESABARI NYASUGUTA***

1. *Yaya e yaya ee x 2*- Hivi sasa, hivi sasa x 2

   *Esabari nyasuguta bare x 2* – Safari ya nyasi ya watahiriwa

   *Makomoke oremire, nchera igoro x 2*- Shangazi amelima, barabarani

   *Akwanigwe, moeti na mogendi x 2*- Asalimiwe na mpita njia na msafiri

2. *Bware yaya, bware yaya x 2* – Hivi sasa, hivi sasa x 2

   *Makomoke oremire, nchera igoro x 2*- Shangazi amelima, barabarani

   *Tiga areme, mboremo bwaborire x 2*- Wacha alime, ni shamba limekosa

   *Akwanigwe, moeti na mogendi x 2*- Asalimiwe na mpita njia na msafiri

3. *Tiga akwanigwe, n'onde otaitongo x 2*- Wacha asalimiwe na mwingine asiyeshamba

   *Makomoke oremire, nchera igoro x 2*- Shangazi amelima, barabarani

   *Akwanigwe, moeti na mogendi x 2*- Asalimiwe na mpita njia na msafiri

## KIAMBATISHO H

## MATINI 8

## *KAMA ENCHAGE*

1. *Kama enchage ee oyaye, kama enchage*- Kamua ng'ombe ee ndio kamua ng;ombe,
   *Oyaye kama enchage k'eng'ombe ekoe omwana* - ndio kamua ng'ombe akupe mwana
   *Oyotakama, oyaye oyotakama, oyaye*- Asiyekamua ndio asiyekamua ndio
   *Oyotakama ebingare biaye bioma*- Asiyekamua ndio watoto wake watakauka.

2. *Ngochia bw'omogaka nganye ebisi, chanire chanire* – Nikiolewa kwa mzee nikamue baadaye, nimeshangaa,nimeshangaa
   *Ngochia bw'omomura nkame nyamasi, chanire chanire*- Nikiolewa kwa mvulana nikamue mengi, nimeshangaa, nimeshangaa
   *Oyotakama, oyaye oyotakama, oyaye*- Asiyekamua ndio asiyekamua ndio
   *Oyotakama ebingae biaye bioma*- Asiyekamua ndio watoto wake watakauka.

3. *Ngochia bw'omogaka nkame omouko, chanire chanire*- Nikiolewa kwa mzee nikamue kipofu, nimeshangaa, nimeshangaa
   *Ngochia bw'omosae nkame nyamasi, chanire chanire* - Nikiolewa kwa kijana nikamue mengi, nimeshangaa, nimeshangaa
   *Oyotakama, oyaye oyotakama, oyaye*- Asiyekamua ndio asiyekamua ndio
   *Oyotakama ebingare biaye bioma*- Asiyekamua ndio watoto wake watakauka.

4. *Kama enchage ee oyaye, kama enchage*- Kamua ng'ombe ee ndio kamua ng;ombe,
   *Oyaye kama enchage, n'emabere mange* – Ndio kamua ng'ombe, ina maziwa mengi
   *Oyotakama, oyaye oyotakama, oyaye*- Asiyekamua ndio asiyekamua ndio
   *Oyotakama ebingare biaye bioma*- Asiyekamua ndio watoto wake watakauka.

5. *Kemunto kama oyaye,Kemunto kama oyaye*- Kemunto kamua ndio, Kemunto kamua
   *Kemunto kama sobo omware yacha*- Kemunto kamua imekuja kwa mtahiriwa
   *Oyotakama, oyaye oyotakama, oyaye*- Asiyekamua ndio asiyekamua ndio
   *Oyotakama ebingare biaye bioma*- Asiyekamua ndio watoto wake watakauka.

6. *Ira ng'ina - yaya, ira ise – yaya, Ira ng'inamoke – yaya* – Mchukue mamake- la, mchukue babake – la, mchukue shangaziye – la'

*Ira eng'iti enene -yaya, ira omware – eeee-* Mchukue joka-la, mchukue mtahiriwa- ndio

*Ira ebikondo- yaya, ira omware- eeee* – Wachukue nyani- la, mchukue mtahiriwa- ndio

*Oyotakama, oyaye oyotakama, oyaye-* Asiyekamua ndio asiyekamua ndio

*Oyotakama ebingare biaye bioma-* Asiyekamua ndio watoto wake watakauka.

## KIAMBATISHO I

## MATINI 9

## *NYAMARUMA*

1. *Nyamaruma ee yaya, nyamaruma x 2* – Akinguruma naam, akinguruma naam

   *Ee yaya nyamaruma bw'eng'ombe ekoe mwana* – Naam akinguruma ng'ombe atakupa mtoto

2. *Koyanire ee yaya, koyanire x 2 ee yaya* – Akinguruma naam, akinguruma,naam

   *Koyanire nakwo okoibora kwaye*- Akinguruma ndiko kuzaa kwake

3. *Tige ebuge ee yaya , tige ebuge x 2ee yaya* – Wacha angurume, naam

   *Tige ebuge tari ange yakarure* – Wacha angurume ametoke mbali

4. *Tige ebuge ee yaya, tige ebuge x 2 ee yaya* – Wacha angurume, naam

   *Tige ebuge n'omware yacha kwoyia* – Wacha angurume amekuja kumchukua mtahiriwa

5. *Tige ebuge ee yaya, tige ebuge x 2 ee yaya* – Wacha angurume naam, wacha angurume naa

   *Tige ebuge yatiga abana baye* – Wacha angurume ameacha watoto wake

6. *Tige ebuge ee yaya, tige ebuge x 2 ee yaya*- Wacha angurume naam, wacha angurume naam

   *Tige ebuge gakorera egesero* – Wacha amgurume anapolia malaloni

7. *Tige ebuge ee yaya, tige ebuge x 2 ee yaya* - Wacha angurume naam, wacha angurume naam

   *Tige ebuge yarure mache ng'umbu* – Wacha angurume ametoka nchi za ng'ambo.

**KIAMBATISHO J**

**MATINI 10**

***AYE SIBA OGENDE***

1. *Nche Sabiri, nchikune, nchitache naende sinsi* – Mimi sabiri, niziguse, nizikanyage tena usiseme
   *Aye siba ogende, ee ogende ogende* – Wewe funga uende, naam uende uende
   *Okarema sinsi* – Ulime usiseme

2. *Kerubo Nyagwoka ochiete orotuba kabuga uui* – Kerubo Nyagwoka alienda toharani akalia uui
   *Aye siba ogende, ee ogende ogende* – Wewe funga uende, naam uende uende
   *Okarema sinsi* – Ulime usiseme

3. *Oyonde ochiete orotuba, akaremia abande* – Mwingine alienda toharani akashajiisha wengine
   *Aye siba ogende, ee ogende ogende* – Wewe funga uende, naam uende uende
   *Okarema sinsi* – Ulime usiseme

4. *Kogoteba nyangi chiato, mani* – Ukisema siri zetu, ulaaniwe
   *Abana bao bakwe, mani* – Watoto wako wafe, ulaaniwe
   *Omogaka oo akwe, mani* – Mume wako afe, ulaaniwe
   *Nyokobiara akwe, mani* – Mavyaa wako afe, ulaaniwe
   *Aye siba ogende, ee ogende ogende* – Wewe funga uende, naam uende uende
   *Okarema sinsi* – Ulime usiseme

## KIAMBATISHO K

## MWONGOZO WA MAHOJIANO

1. Mbona wasichana hutahiriwa katika jamii ya Abagusii?
2. Nyimbo zilikuwa na umuhimu gani katika sherehe za tohara?
3. Ni nyimbo zipi ziliimbwa katika nyakati zifuatazo:
    a) Maandalizi
    b) Tohara yenyewe
    c) Muhula wa kutengwa
    d) Mahafali
4. Je, kwa maoni yako, ni vizuri tuendelee kutahiri wasichana? Toa sababu ya jibu lako.

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY